HAKI KAZI PHDR SW 9/6/05 9:22 AM Page a

JE, TUMEPATA MAENDELEO?

Kutathmini Upunguzaji wa Umaskini Nchini Tanzania

Mwongozo wa Lugha Rahisi wa
Taarifa za Umaskini na Maendeleo ya Watu 2002 na 2003

Kamati ya Utafiti na Uchambuzi

Agosti 2005

HAKI KAZI PHDR SW 9/6/05 9:22 AM Page b

DIBAJI

Upunguzaji wa umaskini umekuwa ni moja ya malengo makuu ya serikali ya Tanzania. Tangu mwaka 2000, Serikali imeanzisha mikakati miwili ya kipindi cha kati ya kupunguza umaskini:

1. Mkakati wa Kupunguza Umaskini wa mwaka 2000
2. Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini Tanzania (MKUKUTA) wa mwaka 2005

Malengo makuu ya Mkakati wa Kupunguza Umaskini wa mwaka 2000 yalikuwa ni:-

- Kupunguza umaskini wa kipato
- Kuboresha uwezo wa watu, kuishi na ustawi
- Kupunguza kuathirika na umaskini

Mkakati huu wa awali ulielezea *sekta za kipaumbele* katika kupunguza umaskini (mf. elimu, afya, n.k.) na kuweka malengo, shughuli na viashirio vya upunguzaji wa umaskini.

MKUKUTA umeboreshwa kutoka katika Mkakati wa kwanza wa Kupunguza Umaskini wa mwaka 2000. MKUKUTA umeandaliwa katika *nguzo kuu tatu*:-

- Ukuaji wa uchumi na kupunguza umaskini wa kipato
- Kuimarisha ubora wa maisha na ustawi wa jamii
- Utawala bora na uwajibikaji

Nguzo zote tatu zinahimiza matokeo kupitia mikakati yake ya utekelezaji. Nguzo ya tatu, utawala bora na uwajibikaji, ni msingi wa nguzo nyingine mbili.

Mchakato wa mashauriano kuhusu MKUKUTA ulifanyika wakati wa mapitio ya Mkakati wa kwanza wa Kupunguza Umaskini. Mapitio hayo yalifanyika kati ya Wiki ya Sera ya Umaskini Oktoba 2003 na ile ya mwaka uliofuatia Novemba 2004.

Mashauriano yaliongozwa na Serikali na wadau wengine, yakiwemo makundi ya kijamii na yale ambayo yalihusisha Umma kwa jumla.



HAKI KAZI PHDR SW 9/6/05 9:22 AM Page ii

Utekelezaji wa mkakati wowote wa upunguzaji wa umaskini ni kusimamia maendeleo yake. Usimamizi wa Mkakati wa kwanza wa Kupunguza Umaskini ulifanywa ili kuangalia kama ulikuwa na athari kwa upunguzaji umaskini – hii ni sawa na kuuliza swali hili: **Je, tumepata maendeleo?** Mnamo mwaka 2001, Serikali ilichapisha Mpango Mkuu wa Ufuatiliaji wa Umaskini, ambao unaelezea Utaratibu wa Ufuatiliaji wa Umaskini. Taarifa ya Umaskini na Maendeleo ya Watu (PHDR) ni moja ya matokeo muhimu ya Utaratibu wa Ufuatiliaji wa Umaskini. Kijitabu hiki kinafupisha Taarifa za Umaskini na Maendeleo ya Watu za mwaka 2002 na 2003[2].

> "Serikali inakusudia kuendelea kuhakikisha kuwepo kwa *uwakilishi wa juu wa maskini na wadau katika utekelezaji, usimamizi na tathmini* ya mkakati wa kupunguza umaskini, na *marudio ya baadaye* ya Waraka wa Mkakati wa Kupunguza Umaskini."
>
> - Waraka wa Mkakati wa Kupunguza Umaskini (PRSP) 2000

Kitabu hiki ni cha mwongozo wa lugha rahisi, maana yake ni kuwa kimeandikwa na kuwasilishwa katika muundo wa lugha rahisi yenye kueleweka. Kimetolewa ili watu wengi zaidi wakipate, waelewe na kutumia taarifa zilizomo. Pamoja na kuwa Mkakati wa kwanza wa Kupunguza Umaskini umeboreshwa na kuwa MKUKUTA, masuala mengi yaliyomo katika kitabu hiki bado ni muhimu katika utaratibu wa sasa wa usimamiaji wa upunguzaji wa umaskini.

Kwa hakika taarifa na mapendekezo kutoka katika ripoti hizi mbili yamesaidia kuelezea maendeleo ya MKUKUTA. Taarifa hizi pia zina mafunzo muhimu na changamoto zinazoweza kutumiwa katika kupanga, kutekeleza na kusimamia MKUKUTA. Hivyo, ni muhimu watu wengi waweze kupata habari hizi katika muundo ambao ni rahisi kuusoma. Maarifa na uelewa wa masuala haya unaweza kusaidia kujenga ushiriki, umiliki na uwajibikaji wa Watanzania wote katika kupunguza umaskini. Taarifa hizi pia zinaweza kuwasaidia wadau wa ngazi zote – jamii, jumuiya ya kiraia, sekta binafsi na serikali – kuendelea kuboresha sera na taratibu za upunguzaji wa umaskini.

Tunawakaribisha wadau wote kuusoma muongozo huu wa lugha rahisi na kuzitumia kwa ufanisi taarifa hizi katika shughuli zao za kupunguza umaskini. Ili kusaidia katika kusoma kitabu hiki, maana ya baadhi ya maneno magumu imeandikwa mwishoni mwa kitabu. Kwa wale watakaohitaji taarifa zaidi, anwani, simu, baruapepe na tovuti zimetolewa kwenye jalada la nyuma.

[2] PHDR inayo fuata inategemewa kutolewa katikati ya mwaka 2005.

HAKI KAZI PHDR SW 9/6/05 9:22 AM Page iii

Yaliyomo

Dibaji i

Yaliyomo iii

Vifupisho iv

1. Utangulizi 1
Taarifa ya Umaskini na Maendeleo ya Watu ni nini? 1
Ni nani aliyefanya utafiti na ulifanyika vipi? 2
Matokeo ya Taarifa ya Umaskini na Maendeleo ya Watu yanaweza kutumiwa vipi? 2
Kitabu hiki kinatuambia nini na mpangilio wake ukoje? 2

2. Kiwango cha Umaskini Nchini Tanzania Kikoje? 4
Umaskini wa Kipato: Ukuaji, Ajira na Barabara 5
Elimu 7
Kuishi, Lishe na Afya 9
Maji na Usafi 13
Kuathirika na Umaskini 16
Uhusishaji wa Umaskini na Mazingira 17
Utawala 19
Muhtasari wa Kiwango cha Umaskini Tanzania 20

3. Mada Muhimu za Umaskini 24
Umaskini Mijini 24
Uhusishaji wa Sera za Jumla na Umaskini 26
Athari za Umaskini na Uangalizi wa Jamii 31
Faida Inayotarajiwa 34
Masuala ya Utawala Yanayoathiri Umaskini na Athari Zake 37
Kilimo 41

4. Changamoto, Hitimisho na Mapendekezo 46
Masomo na Changamoto 46
Hitimisho 47
Mapendekezo 49

Maana ya Baadhi ya Maneno Magumu 51

HAKI KAZI PHDR SW 9/6/05 9:22 AM Page iv

Vifupisho

ASDP	Mpango wa Maendeleo ya Sekta ya Kilimo
ASDS	Mkakati wa Maendeleo ya Sekta ya Kilimo
GDP	Pato la Taifa
HIV+	Kuwa na Virusi vya UKIMWI
IMCI	Uthibitisho Unganifu wa Magonjwa ya Kitoto
JFMA	Mkataba wa Usimamizi wa Pamoja wa Misitu
LGRP	Programu ya Maboresho ya Serikali za Mitaa
LSRP	Programu ya Urekebishaji wa Sekta ya Sheria
MEMKWA	Mkakati wa Elimu ya Msingi kwa Waliokosa
MKUKUTA	Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini Tanzania
MTEF	Muundo wa Matumizi ya Muda wa Kati
NGO	Asasi Isiyo ya Serikali
PAYE	Lipa Kadiri Unavyoingiza
PEDP / MMEM	Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Msingi
PER	Mapitio ya Matumizi ya Umma
PFM	Usimamizi Shirikishi wa Misitu
PHDR	Taarifa ya Umaskini na Maendeleo ya Watu
PRS / MKU	Mkakati wa Kupunguza Umaskini
PRSP	Waraka wa Mkakati wa Kupunguza Umaskini
PSLE	Mtihani wa Kumaliza Elimu ya Msingi
R&AWG	Kundi la Utafiti na Uchambuzi
RDS	Mkakati wa Maendeleo Vijijini
TAKURU	Taasisi ya Kuzuia Rushwa
TzPPA	Tathmini Shirikishi ya Umaskini Tanzania
VETA	Vituo vya Elimu ya Ufundi
VVK	Vyama vya Kiraia
VVU	Virusi vya UKIMWI
WMA	Maeneo ya Usimamiaji wa Wanyamapori

HAKI KAZI PHDR SW 9/6/05 9:22 AM Page 1

1. Utangulizi

Sura hii inaelezea:

- Taarifa ya Umaskini na Maendeleo ya Watu ni nini?
- Ni nani aliyefanya utafiti na ulifanyika vipi?
- Namna matokeo yanavyoweza kutumika
- Namna kitabu hiki kilivyopangwa

TAARIFA YA UMASKINI NA MAENDELEO YA WATU NI NINI?

Malengo, Shughuli na Viashirio

Malengo: Wazo lililo wazi la kila unachokusudia kufikia.

Shughuli: Hatua utakazopitia kufikia malengo yako.

Viashirio: Vitu utakavyopima kujua kama shughuli zako zimefikia malengo yako.

Taarifa ya Umaskini na Maendeleo ya Watu ni moja ya matokeo muhimu ya Utaratibu wa Ufuatiliaji wa Umaskini. Hii ni nyenzo inayotumiwa na serikali kutafiti kama Mkakati wa kwanza wa Kupunguza Umaskini una athari zozote katika kupunguza umaskini. Upimaji wa kupunguza umaskini unajumuisha utumiaji wa viashirio ambavyo vimeonyeshwa kwenye Mkakati wa kwanza wa Kupunguza Umaskini. Mkakati huu unaelezea maeneo ya vipaumbele katika kupunguza umaskini na kupanga malengo, shughuli na viashirio vya kupunguza umaskini (angalia kisanduku). Taarifa ya Umaskini na Maendeleo ya Watu inachambua kiwango cha umaskini katika sekta za kipaumbele kwa kutumia viashirio hivi. Ufuatiliaji wa maendeleo ya upunguzaji wa umaskini ni sehemu muhimu ya utekelezaji wa Mkakati wa kwanza wa Kupunguza Umaskini na Taarifa ya Umaskini na Maendeleo ya Watu ni sehemu ya utaratibu huu.



HAKI KAZI PHDR SW 9/6/05 9:22 AM Page 2

NI NANI ALIYEFANYA UTAFITI NA ULIFANYIKA VIPI?

NANI: Utafiti huu ulifanywa na Kundi la Utafiti na Uchambuzi (R&AWG), ambalo ni sehemu ya Utaratibu wa Ufuatiliaji wa Umaskini. Kundi hili linatoa uchambuzi kusaidia kueleweka kwa kiasi na sababu za umaskini nchini na juu ya athari za sera ya upunguzaji wa umaskini.

VIPI: Watafiti wanachambua taarifa zilizotoka katika ripoti nyingi zinazotolewa na serikali, asasi zisizo za serikali, vyuo vikuu na taasisi za kimataifa (angalia kisanduku). Ripoti hizi hujumuisha aina mbili za taarifa kuhusu kiwango cha umaskini katika maeneo mbalimbali yaliyopewa kipaumbele. Aina moja hujumuisha hoja na idadi (yaani takwimu) na hutumiwa kupima viashirio vya ufuatiliaji wa umaskini. Taarifa ya Umaskini na Maendeleo ya Watu 2002 inatumia aina hiyo ya taarifa peke yake. Hata hivyo, hoja na idadi havitoshi katika kuuelewa umaskini. Kujua maisha ya watu pia kunahitajika namna wanavyouona na kuelewa umaskini na unavyosababishwa kulingana na uzoefu wao. Aina hiyo ya pili ya taarifa ilitumiwa, pamoja na takwimu, kwenye Taarifa ya Umaskini na Maendeleo ya Watu 2003. Maelezo yalichukuliwa kutoka kwenye Tathmini Shirikishi ya Umaskini Tanzania (TzPPA) na yalitumiwa kuchambua athari za umaskini kwa watu. Kundi la Utafiti na Uchambuzi (R&AWG) pia liliyakabidhi mashirika mengine kufanya utafiti kupata taarifa zaidi juu ya mada muhimu za umaskini, kama athari za umaskini, utawala na kilimo. Aidha, R&AWG ilifanya jitihada maalum kusaidia uwezo wa watafiti wa ndani kuchambua umaskini kwa kuwa na watafiti wanaoshiriki katika ngazi zote za tafiti hizi.

Vyanzo vikuu vitatu vya Ripoti:

- *Takwimu za kila siku* zinazokusanywa na vijiji, mikoa na idara za serikali (mfano, kiasi cha vifo vya watoto wachanga kutoka katika Wizara ya Afya)
- *Tafiti/sensa* zinazofanywa na Shirika la Takwimu la Taifa (mfano, Ukaguzi wa Bajeti ya Makazi)
- *Tafiti maalum* zilizofanywa na watafiti mbalimbali wa asasi zisizo za serikali, vyuo vikuu, na taasisi za kimataifa

MATOKEO YA TAARIFA YA UMASKINI NA MAENDELEO YA WATU YANAWEZA KUTUMIWA VIPI?

Kusudi moja la ripoti hii ni kutoa taarifa za kutumainiwa za upunguzaji wa umaskini kwa umma kwa wakati unaofaa. Taarifa hizi zinaweza kutumiwa na nyanja zote za serikali, jumuiya za wananchi, sekta binafsi na jumuiya za vijijini. Wadau wote wanaweza kujadili taarifa hizi na kuzitumia katika:

- Uboreshaji wa utaratibu wa ufuatiliaji wa umaskini na kutafuta ufumbuzi
- Uboreshaji wa mchakato wa ufuatiliaji wa umaskini na viashirio
- Uboreshaji wa ukusanyaji wa takwimu hususani kwenye maeneo yasiyo na takwimu kamili
- Kushawishi uundaji wa sera
- Kubainisha masuala muhimu ambayo ni lazima yatekelezwe

Taarifa ya Umaskini na Maendeleo ya Watu ni muhimu kwa:

- Uchambuaji wa viwango na mwelekeo wa umaskini
- Utoaji mzuri wa taarifa kwa umma na kwa wakati unaofaa
- Uwezeshaji wa ufanyaji maamuzi juu ya mabadiliko yoyote ya mikakati ya upunguzaji wa umaskini

KITABU HIKI KINATUAMBIA NINI NA MPANGILIO WAKE UKOJE?

Kitabu hiki ni mwongozo wa lugha rahisi wa Taarifa za Umaskini na Maendeleo ya Watu za mwaka 2002 na 2003. Taarifa halisi za Umaskini na Maendeleo ya Watu ni ndefu na zina uchambuzi zaidi. Hata hivyo, kitabu hiki kinafupisha taarifa zilezile katika namna rahisi kiasi cha kuweza kuwafikia watu wengi.

HAKI KAZI PHDR SW 9/6/05 9:22 AM Page 3

Sehemu ya kwanza ya kitabu hiki inaonyesha uchambuzi wa kiwango cha umaskini kulingana na viashirio vilivyoonyeshwa kwenye Mkakati wa kwanza wa Kupunguza Umaskini. Pia, kinatumia viashirio vya umaskini vilivyorekebishwa ambavyo vilitolewa mapema mwaka 2003 na kuviacha viashirio vilivyotumiwa mwaka uliopita. Maeneo ya vipaumbele yaliyotumiwa kuchambua kiwango cha umaskini ni:

1. Umaskini wa kipato
2. Elimu
3. Kuishi, lishe na afya
4. Maji na usafi
5. Kuathirika na umaskini
6. Uhusishaji wa umaskini na mazingira
7. Utawala

Sehemu ya pili ya kitabu hiki inaonyesha uchambuzi wa mada muhimu za umaskini zilizoshughulikiwa katika Taarifa za Umaskini na Maendeleo ya Watu zote mbili. Mada hizi ni:

- Umaskini wa mijini
- Uhusishaji wa sera za jumla na umaskini
- Athari za umaskini na uangalizi wa jamii
- Faidi inayotarajiwa
- Utawala
- Kilimo

Sehemu ya mwisho ya kitabu hiki ina muhtasari wa changamoto, masuala muhimu, na mapendekezo yanayotokana na uchambuzi wa viashirio na mada muhimu za umaskini. Mwisho kitabu kinamalizika kwa kuwa na orodha ya maneno magumu inayotoa maana zake.

HAKI KAZI PHDR SW 9/6/05 9:22 AM Page 4

2. Kiwango cha Umaskini Nchini Tanzania Kikoje?

Sura hii inaelezea kiwango na mwelekeo wa umaskini kulingana na uchambuzi wa viashirio vya upunguzaji wa umaskini katika maeneo ya vipaumbele. Baadhi ya viashirio vilivyorekebishwa na/au vipya vimejumuishwa, hivyo utaona katika sehemu zinazofuata kuwa baadhi havina malengo. Hii ni kwa sababu wakati taarifa hizi zinaandikwa, malengo yalikuwa bado hayajapangwa. Hata hivyo tangu mwaka 2003 malengo yalishapangwa, na baadhi yanatumiwa katika MKUKUTA.

Katika sura hii, mwelekeo wa kipindi cha Mkakati wa Kupunguza Umaskini (2000-2003) na ule wa miaka ya 1990 umeonyeshwa. Hii inasaidia kutoa sura ya jumla ya mwelekeo wa kupunguza umaskini kulingana na wakati. Sura hii pia inaangalia kama malengo yanakaribia kufikiwa na kupendekeza marudio ya sera na njia za ufuatiliaji. Jedwali la hapo chini linaonyesha maeneo gani ya vipaumbele yaliyoshughulikiwa katika ripoti za miaka 2002 na 2003:

Taarifa ya Umaskini na Maendeleo ya Watu 2002	**Taarifa ya Umaskini na Maendeleo ya Watu 2003**
Umaskini wa Kipato, ukijumuisha Ukuaji wa Uchumi na Barabara	Umaskini wa Kipato, ukijumuisha Ukuaji wa Uchumi, Ajira na Barabara
Ajira	Elimu
Elimu	Kuishi, Lishe na Afya
Kuishi	Maji na Usafi
Lishe	Kuathirika na Umaskini
Maji	Uhusishaji wa Umaskini na Mazingira
	Utawala

Kulingana na jedwali la hapo juu maeneo matatu mapya ya vipaumbele yalijumuishwa kwenye ripoti ya mwaka 2003:

1. Kuathirika na Umaskini
2. Uhusishaji wa Umaskini na Mazingira
3. Utawala

Maeneo mengine ya vipaumble yanaonekana katika ripoti zote mbili. Sehemu zifuatazo zinajumuisha uchambuzi wa ripoti zote mbili juu ya viashirio vya kiwango cha umaskini katika maeneo ya juu ya vipaumbele.

HAKI KAZI PHDR SW 9/6/05 9:22 AM Page 5

Umaskini wa Kipato: Ukuaji, Ajira na Barabara

Sehemu hii inaangalia viashirio vinavyopima umaskini wa kipato. Watafiti wametumia viashirio hivi kuchambua kiwango na mwelekeo katika ukuaji wa uchumi, ajira na barabara. Majedwali ya hapo chini yanatoa muhtasari wa viashirio vilivyotumiwa, malengo na kiwango cha kila kiashirio. Baada ya majedwali, kuna muhtasari wa maendeleo ya upunguzaji wa umaskini katika eneo hili la kipaumbele, ikiwa ni pamoja na masuala ya sera na mapendekezo. Taarifa nyingi ni zile zile katika ripoti zote mbili kwani hakukuwa na takwimu mpya kwa baadhi ya viashirio.

V*iashirio vyenye malengo (vya mwaka 2003):*

Viashirio	**Malengo ya 2003**	**Kiwango**
Asilimia ya watu walio chini ya mstari wa umaskini wa mahitaji ya msingi	30%	• 36% mnamo mwaka 2000/01
Asilimia ya watu walio chini ya mstari wa umaskini wa chakula	16%	• 19% mnamo mwaka 2000/01
Kiwango cha ukuaji wa Pato la Taifa	6%	• Juu kidogo ya 6% mnamo mwaka 2002
Kiwango cha ukuaji wa kilimo	5%	• 5% ya ukuaji ilifikiwa mnamo mwaka 2001 na 2002
Mfumuko wa bei ya chakula katika maeneo ya mijini	4%	• 4.1% mwaka 2002

Viashario visivyo na malengo (vya mwaka 2003):[3]

Viashirio	**Malengo ya 2003**	**Kiwango**
Asilimia ya wakulima wadogo waliosema kuwa kuwepo au gharama ya usafiri ni kikwazo kwa masoko	-	• Hakuna taarifa zilizopatikana
Asilimia ya wakulima wadogo ambao walitaka mikopo lakini hawakuweza kuitumia katika mwaka huo	-	• Hakuna taarifa zilizopatikana
Asilimia ya wakulima wadogo walioeleza kuridhishwa na huduma za kilimo	-	• Hakuna taarifa zilizopatikana
Asilimia ya wilaya zilizoarifiwa kuwa na upungufu wa chakula	-	• 39% zilikuwa na upungufu wa chakula mwaka 2003
Kilomita za barabara zilizofanyiwa ukarabati kwa awamu	-	• km 663 mwaka 2002/03 – 1% ya barabara zote
Kilomita za barabara zilizofanyiwa ukarabati wa mara kwa mara	-	• km 12,405 mwaka 2002/03 - 16% ya barabara zote
Asilimia ya watu wenye umri wa kufanya kazi ambao kwa sasa hawana ajira	-	• 5% katika mwaka 2000/01 (kwa kutumia tafsiri ya kimataifa ya kutoajiriwa)
Asilimia ya watu wenye umri kati ya miaka 15-24 ambao kwa sasa hawana ajira katika maeneo ya mijini	-	• 28% katika mwaka 2000/01 (kwa kutumia tafsiri ya kimataifa ya kutoajiriwa)

[3] Tafadhali zingatia kuwa malengo yalikwisha wekwa baada ya kuandikwa taarifa hii.

HAKI KAZI PHDR SW 9/6/05 9:22 AM Page 6

Hitimisho na Mapendekezo

Kumekuwepo na kupungua kidogo kwa umaskini wa kipato katika miaka ya 1990, hususani maeneo ya vijijini. Ukuaji wa uchumi katika kipindi cha miaka ya 1991-2001 ulikuwa mdogo, na kulikuwa na ongezeko la tofauti kati ya matajiri na maskini. Hata hivyo, kuongezeka kwa ukuaji wa uchumi kulisababisha msingi mzuri wa kipindi kirefu cha upunguzaji wa umaskini. Ukuaji wa uchumi, ukuaji wa kilimo na mfumuko wa bei vinakusudiwa kusaidia ufikiaji wa malengo ya Mkakati wa Kupunguza Umaskini. Ukuaji wa uchumi ni muhimu katika kuongeza pato la vijijini. Sekta nyingine (mf. madini) zimekua sana, lakini zinachangia asilimia ndogo ya Pato la Taifa (GDP) na kutoa ajira ndogo. Uwekezaji kwenye kilimo ulikuwa mdogo ingawa kinafanya 50% ya Pato la Taifa. Uzalishaji wa mazao ya biashara uliongezeka, hata hivyo, pato la nje lililokuwa na mazao haya lilishuka kwa sababu ya kupungua kwa bei na kushuka kwa kiasi cha uuzaji wa mazao ya ndani katika soko la dunia. Uwezo wa kupata mikopo wakulima wadogo ulionekana kupungua kuanzia mwishoni mwa miaka ya 1990 uliotokana na urekebishaji wa uchumi, japokuwa hakuna taarifa ya moja kwa moja ya kiashirio hiki.



Hali ya barabara nyingi ni mbovu, hususani barabara za wilayani. Programu ya ukarabati iliyoonyeshwa kwenye Waraka wa Mkakati wa Kupunguza Umaskini (PRSP) haikufanywa kwani fedha zilitumika kutengeneza barabara nyingine. Kiwango cha utengenezaji na ukarabati wa barabara kilibaki kuwa kidogo.

Kukosekana kwa ajira kunaonekana zaidi katika maeneo ya mijini na ni kiwango kikubwa kwa wanawake kuliko wanaume. Kukosa ajira kwa vijana ni kwingi mijini, ingawa jumla ya ajira ilipanda miaka ya 1990. Ajira katika serikali na mashirika imepungua, wakati katika sekta binafsi hasa mijini imeongezeka. Ukosefu wa nafasi za kiuchumi vijijini unatokana na kuwepo kwa "kiwango cha chini cha ajira." Hii ina maana ya kuwa watu wanajihusisha sana na kilimo cha kujikimu.

HAKI KAZI PHDR SW 9/6/05 9:22 AM Page 7

Kukosekana kwa Ajira:
Masuala Muhimu

- Changamoto kubwa ya Mkakati wa kwanza wa Kupunguza Umaskini ni kuongeza fursa za kiuchumi kwa maskini vijijini na mijini
- Kiwango cha juu cha kukosekana kwa ajira kwa wenye elimu ya msingi na sekondari mijini kinathibitisha kuwa ujuzi wao hautoshi kuwapatia ajira
- Programu za uongezaji wa ujuzi wa vijana wasio na ajira lazima zianzishwe ili kupata ajira rasmi

Sera kuu inayotakiwa hapa ni **namna ambayo ukuaji wa uchumi utakavyosambazwa kwa maskini, hususani vijijini**. Kilimo ni muhimu kwani watu wengi wa vijijini wanakitegemea kwa ajili ya ajira na uhakika wa chakula. Kiwango cha juu cha ukuaji wa kilimo kwa hiyo kinahitajika kupewa kipaumbele. Kiasi kidogo cha uwekezaji katika kilimo na mabadiliko katika bei ya mazao ni tatizo. Wakulima wadogo pia wanatakiwa kuwa na uwezo wa kupata mikopo. Uwekezaji katika sekta nyingine, mf. madini na uzalishaji, unatakiwa kusaidia uchumi mzima hasa kwa kutoa nafasi zaidi za ajira.

Elimu

Sehemu hii inaangalia viashirio vinavyopima kiwango cha elimu nchini Tanzania. Watafiti wametumia viashirio hivi kuchambua kiwango na mwelekeo wa uandikishwaji wa watoto katika shule za msingi na sekondari, uwiano wa kijinsia, ubora wa elimu na kujua kusoma na kuandika. Majedwali ya hapo chini yanatoa muhtasari na viashirio vilivyotumiwa, malengo na kiwango cha kila kiashirio. Baada ya jedwali kuna muhtasari wa maendeleo ya upunguzaji umaskini katika eneo hili la kipaumbele, ikiwa ni pamoja na masuala ya sera na mapendekezo. Taarifa nyingi ni sawa katika ripoti zote mbili kwani hakukuwa na takwimu mpya zilizopatikana kwa baadhi ya viashirio.

Viashirio vyenye malengo (vya mwaka 2003):

Viashirio	**Malengo ya 2003**	**Kiwango**
Uandikishwaji wa watoto katika shule za msingi	90%	• Uandikishwaji katika shule za msingi mwaka 2003 ulikuwa 89%
Uwiano wa wasichana/wavulana katika shule za msingi	100/100	• 95/100 ya wanafunzi wa shule za msingi mwaka 2003 walikuwa ni wasichana
Idadi ya wanafunzi walioacha shule za msingi	3%	• Idadi ya wanafunzi walioacha ni kiasi cha 5% kukiwa na kiasi kidogo cha maendeleo
Asilimia ya wanafunzi wanaofaulu mtihani wa kumaliza elimu ya msingi (PSLE)	50%	• 29% ya wanafunzi walifaulu mtihani (PSLE) katika mwaka 2001 ambao ni wachache
Idadi ya wanafunzi kutoka darasa la 7 kwenda kidato cha 1	28%	• 19% mwaka 2003
Uwiano wa wasichana/wavulana katika shule za sekondari	90/100	• 84/100 ya wanafunzi wa shule za sekondari mwaka 2003 walikuwa ni wasichana
Idadi ya wanaojua kusoma na kuandika wenye umri zaidi ya miaka 15	100% ifikapo 2010	• 71% katika mwaka 2000/01

HAKI KAZI PHDR SW 9/6/05 9:22 AM Page 8

Viashirio visivyo na malengo (vya mwaka 2003):[4]

Viashirio	Malengo ya 2003	Kiwango
Idadi ya wanafunzi wanaomaliza darasa la 7	-	• 72% ya wanafunzi waliomaliza darasa la 7
Wanaojua kusoma na kuandika wenye umri wa miaka 15-24	-	• 82% katika mwaka 2000/01

Hitimisho na Mapendekezo

Kumekuwepo na ongezeko kubwa la uandikishwaji wa watoto katika shule za msingi katika miaka mitatu iliyopita kwa sababu ya Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Msingi (MMEM) na kufutwa kwa ada ya shule. Uandikishwaji ulikuwa zaidi ya malengo ya Mkakati wa kwanza wa Kupunguza Umaskini ya mwaka 2003. Watoto wanaingia shuleni katika umri mdogo, na kuna ongezeko la idadi ya watoto wanaokwenda shuleni. Kuna uwiano sawa wa wavulana na wasichana wenye umri wa miaka 7 wanaoandikishwa, hata hivyo, kuna wavulana wakubwa zaidi ya wasichana wanaoandikishwa. Hii inaonyesha kuwa ni vigumu kwa wasichana wenye umri mkubwa kuanza shule. Kuna wasichana wachache sana wanaokwenda shuleni katika ngazi zote na mwelekeo huu unazidi kuongezeka. Itakuwa vigumu kufikia malengo ya Mkakati wa kwanza wa Kupunguza Umaskini ya usawa katika uandikishwaji wa wasichana na wavulana hadi mwaka 2005.

Elimu:
Masuala Muhimu

- Ubora wa elimu unaathiriwa na:
  - Idadi ya wanaoandikishwa
  - Shule zisizotosha
  - Mitaala ya zamani
  - Athari ya VVU/UKIMWI kwa walimu
- Kutokuwepo kwa usawa wa kijinsia, hususani sekondari na elimu ya juu
- Watoto wenye umri mkubwa na wasio shuleni na watu wazima wasiojua kusoma wametengewa
- Programu za elimu kwa waliokosa kama Mkakati wa Elimu ya Msingi kwa Waliokosa (MEMKWA) lazima zipanuliwe

Ubora wa elimu ya msingi bado ni mdogo, licha ya kulikuwa na maendeleo madogo katika kiwango cha kufaulu cha mtihani wa kumaliza elimu ya msingi (PSLE) na idadi ya wanaoingia elimu ya sekondari. Wasichana wanafanya vibaya sana ikilinganishwa na wavulana katika mitihani ya PSLE. Pia, kumekuwepo na idadi kubwa ya waliorudia elimu ya msingi mwaka 2003. Uwezo wa shule za sekondari umeongezeka katika miaka ya hivi karibuni, lakini si mkubwa wa kuweza kuchukua wanafunzi wote wanaofaulu mitihani hiyo. Kiasi cha 12% tu ya wenye umri huo huingia shule za sekondari.

Ingawa kutokujua kusoma miongoni mwa Watanzania wenye umri wa miaka 15-24 ni kwa chini sana kuliko watu wazima, bado ni zaidi ya 20% vijijini na 25% miongoni mwa wanawake wa vijijini. MMEM umeahidi kuendeleza jamii ya watu wazima wanaojua kusoma katika siku za usoni. Hata hivyo, watoto wengi walikosa kupata fursa ya kujiunga na shule katika miaka ya 1990 na sasa ni wazee mno kufaidika na elimu rasmi.

Kwa upande wa sera, kuongezeka kwa sasa kwa wanafunzi katika shule za msingi kumesababisha matatizo mengi katika miundombinu ya shule, mahitaji shuleni na walimu. MMEM unaendelea kuyashughulikia maeneo haya. Hata hivyo, mikakati ya kuondoa vikwazo katika uingizaji na maendeleo mazuri ya wasichana lazima itekelezwe. Pia, watoto maskini na yatima wanaweza kuhitaji ruzuku ili waweze kumaliza shule ya msingi. Elimu isiyo rasmi kwa watoto wasiokuwa shuleni na watu wazima wasiojua kusoma haitoshelezi.

[4] Tafadhali zingatia kuwa malengo yalikwisha wekwa baada ya kuandikwa taarifa hii.

Malengo ya Mkakati wa kwanza wa Kupunguza Umaskini ya kumaliza tatizo la kuwa na idadi ya watu wasiojua kusoma hadi kufikia 2010 haitafikiwa, isipokuwa Mkakati mpya wa Elimu ya Watu Wazima na isiyo Rasmi utagharamiwa kwa makini na kutekelezwa. Tathmini kubwa ya mitaala ya shule huchelewa sana. Inahitaji utafiti wa kina wa kujua kwanini wasichana wana kiwango hicho kibaya cha kufaulu ikilinganishwa na wavulana katika shule za msingi. Pia, uzingatie mapendekezo kutoka kwa wanafunzi wa zamani kuhusu kujumuisha maarifa na ujuzi unaofaa kwa ajili ya ajira.



Kuishi, Lishe na Afya

Sehemu hii inaangalia viashirio vinavyopima kuishi, lishe na afya. Sehemu ya kwanza ya chini inaonyesha viashirio vya kuishi na lishe. Sehemu hiyo inafuatiwa na uchambuzi wa viashirio vya utoaji wa huduma za afya. Sehemu ya mwisho inajadili sera ya jumla na mapendekezo ya kuishi, lishe na afya. Taarifa nyingi ni zile zile katika taarifa zote mbili kwani hakukuwa na takwimu mpya zilizopatikana kwa baadhi ya viashirio.

KUISHI NA LISHE

Jedwali la hapo chini linatoa muhtasari wa viashirio vilivyotumika kupima kuishi na lishe, malengo na viwango vya kila kiashirio. Baada ya jedwali, kuna muhtasari wa maendeleo katika eneo hili la kipaumbele.

Viashirio vyenye malengo (vya mwaka 2003):

Viashirio	Malengo	Kiwango
Kiwango cha vifo vya watoto wachanga	Vifo 85 kati ya watoto 1,000 waliozaliwa ifikapo mwaka 2003	• Vifo 99 kati ya watoto 1,000 waliozaliwa kati ya mwaka 1994-1999
Kiwango cha vifo vya watoto chini ya miaka 5	Vifo 127 kati ya watoto 1,000 waliozaliwa ifikapo mwaka 2003	• Vifo 147 kati ya watoto 1,000 waliozalwa kati ya mwaka 1994-1999
Umri wa kuishi	Miaka 52 ya kuishi ifikapo mwaka 2010	• Miaka 50 (kulingana na taarifa za maeneo ya utafiti) • Kiwango cha mwisho cha taifa kilikadiriwa kuwa miaka 52 (sensa ya 1988)
Asilimia ya watoto chini ya miaka 5 waliodumaa	20% ifikapo 2010	• 44% ya watoto walidumaa mwaka 1999 (inaonyesha wanapata lishe duni)

Viashirio visivyo na malengo (vya mwaka 2003):[5]

Viashirio	Malengo	Kiwango
Uwiano wa vifo vya watoto wachanga kwa familia maskini na tajiri	-	• Watoto wachanga waliozaliwa na mama maskini wana 25% ya uwezekano mkubwa wa kufa kabla ya kufikia mwaka 1 kuliko wale wa matajiri
Badiliko la asilimia ya idadi ya vifo vya watoto chini ya miaka 5 kwa sababu ya malaria	-	• Hakuna takwimu za kitaifa, hata hivyo, taarifa kutoka katika maeneo ya utafiti zinaonyesha mabadiliko madogo katika kiashirio hiki
Kiwango cha wenye VVU kwa wenye umri wa miaka 15-24	-	• 8% ya wanaume (2001) • 13% ya wanawake (2001)
Asilimia ya watoto waliozaliwa na akina mama wenye VVU na kuambukizwa	-	• Hakuna takwimu - zinategemewa mwaka 2006
Idadi ya uzazi	-	• Watoto 5.6 kwa mwanamke (1999)

[5] Tafadhali zingatia kuwa malengo yalikwisha wekwa baada ya kuandikwa taarifa hii.

HAKI KAZI PHDR SW 9/6/05 9:22 AM Page 11

Hitimisho

Vifo vya watoto wadogo na wachanga havikupungua katika miaka ya 1990, lakini vilipungua katika maeneo ya utafiti kuanzia mwaka 2000. Maeneo haya yalizitekeleza programu za Uthibitisho Unganifu wa Magonjwa ya Kitoto (IMCI). Hata hivyo, hadi sasa hakuna tathmini iliyofanywa. Malengo ya Mkakati wa kwanza wa Kupunguza Umaskini ya vifo 85 kwa kila watoto wanaozaliwa hai 1,000 itakuwa ngumu kufikiwa kwani maelfu ya watoto wachanga watakuwa wameambukizwa VVU na mama zao. Kiwango cha uambukizwaji wa VVU kimeendelea kuongezeka na hakuna dalili za kupungua. Kati ya watu milioni 2 waliokadiriwa kuwa na VVU, 700,000 kati yao wana UKIMWI. Umri wa kuishi umeshuka tangu mwaka 1988 kwa sababu ya VVU/UKIMWI.

Malaria bado ni chanzo kikuu cha vifo vya watoto chini ya miaka 5, na hili halikupungua katika miaka ya 1990. Hata hivyo, maeneo yaliyoonekana kuwa na vifo vichache vya watoto yalionyesha pia kuwa na vifo vichache vilivyosababishwa na malaria. Katika miaka ya 1990 kumekuwa na uboreshwaji mdogo wa lishe kwa watoto chini ya miaka 5. Lishe ilikuwa duni vijijini na miongoni mwa maskini. Uhaba wa chakula na VVU/UKIMWI huchangia katika utapiamlo. Idadi ya uzazi ilipungua katika miaka ya 1990, japokuwa vijijini na kwa maskini ilibaki kuwa juu; ujauzito miongoni mwa wasichana pia ulibaki juu.

Afya ya Watoto: Masuala Muhimu

- Kupungua kwa huduma za uzazi zilizofanywa na wauguzi wenye ujuzi
- Ongezeko dogo katika vifo vya watoto wachanga na watoto wadogo kwa sababu ya VVU/UKIMWI
- Idadi ya vifo vya watoto ni ndogo kwa matajiri, lakini kubwa kwa wenye kipato cha ngazi zote
- Upataji wa malaria wa watoto haujapungua
- Utapiamlo kwa watoto bado ni mkubwa
- Uangalizi mzuri wa maisha ya watoto unahitajika, yaani kutatua umaskini na masuala ya afya kwa wakati mmoja

UTOAJI WA HUDUMA ZA AFYA

Utoaji wa huduma za afya ulikuwa eneo jipya la kipaumbele katika ripoti ya mwaka 2003. Hata hivyo, viashirio viwili katika jedwali la kwanza vilikuwa katika ripoti zote mbili (mwaka 2002 viliingizwa kwenye "kuishi"). Baada ya jedwali, kuna muhtasari wa maendeleo ya eneo hili la kipaumbele.

Viashirio vyenye malengo (vya mwaka 2003):

Viashirio	Malengo	Kiwango
Uzazi uliofanywa na daktari, muuguzi au mkunga mwenye ujuzi	80% ifikapo 2010	• 36% mwaka 1999
Chanjo zilizotolewa kwa donda koo, pepopunda na polio	85% ifikapo 2003	• 89% ya watoto walipata chanjo mwaka 2002

Viashirio visivyo na malengo (vya mwaka 2003):[6]

Viashirio	Malengo	Kiwango
Kiwango cha mtu kutibiwa kwa mwaka (wagonjwa wasiolala hospitali)	-	• Mara 1.3 kwa mwaka kwa huduma za serikali • Mara 2.3 kwa mwaka pamoja na huduma za binafsi
Kiwango cha kutosha kwa mtumiaji wa huduma za afya	-	• 66% ya watumiaji wa huduma za serikali walitosheka • 71% ya watumiaji wa huduma za serikali na binafsi walitosheka
Jumla ya waliokubali uzazi wa mpango	-	• Kiasi cha watu milioni 1.5 walitumia uzazi wa mpango (2001)
Uzazi unaofanywa katika huduma za afya	-	• 44% mwaka 1999
Tiba ya ugonjwa wa kifua kikuu	85% ifikapo 2004	• Kiwango cha umaliziaji wa tiba ya kifua kikuu kiliongezeka kutoka 76% hadi 81% kati ya mwaka 1998-2001

Hitimisho

Mwelekeo wa huduma za afya unaonyesha sura mchanganyiko katika kipindi cha miaka ya 1990. Kiwango cha utoaji wa huduma kwa huduma zinazowezeshwa na programu maalum kilipanda mnamo mwaka 2000. Kiwango cha mtu kutibiwa (wagonjwa wasiolala hospitali) kiliongezeka kwa 47% kati ya mwaka 2000 na 2002. Hata hivyo, moja ya tatu ya watumiaji walilalamikia huduma zinazotolewa na vituo vya afya vya serikali. Walilalamikia matatizo kama ya muda wa kusubiri na uhaba wa wafanyakazi na dawa.

Asilimia ya uzazi uliofanywa na wafanyakazi wenye ujuzi na ule uliofanywa kwenye vituo vya afya ilishuka na tofauti kati ya maeneo ya mijini na vijijini iliongezeka. Idadi ya watu waliotumia uzazi wa mpango iliongezeka kwa 8.4% kati ya mwaka 2000-2001.

Tanzania ina kiasi kikubwa cha chanjo ya watoto. Kiwango cha chanjo kilikuwa 90% katika mwaka 2002, ambayo ni zaidi ya lengo la Mkakati wa kwanza wa Kupunguza Umaskini. Hata hivyo, baadhi ya wilaya zina kiwango kidogo, hasa maeneo ya vijijini. Watoto wa matajiri wana uwezo mkubwa wa kupata kuliko watoto wa maskini.

Kifua kikuu ni chanzo kikubwa cha vifo vya watu wazima, na 44% ya wagonjwa wa kifua kikuu wana VVU. Hata hivyo, kuongezeka kwa kiwango cha umaliziaji wa tiba ya kifua kikuu kunatia moyo.

Masuala ya Sera na Mapendekezo ya Kuishi, Lishe na Afya

Watu maskini na wale wa vijijini ndio hasa wanaotaabika katika kuishi, lishe na upataji wa huduma za afya. Ni muhimu kuhakikisha kuwa huduma za afya zinapatikana na ni rahisi kwa watu wa vijijini na maskini. Malipo yasiyo rasmi na gharama zisizo za moja kwa moja ni kikwazo kwa utumiaji wa huduma

[6] Tafadhali zingatia kuwa malengo yalikwisha wekwa baada ya kuandikwa taarifa hii.

hizi. Pendekezo la uanzishaji wa kulipia katika vituo vidogo vya afya litaongeza zaidi gharama wanayokabiliana nayo watumiaji na unaweza kuwa na madhara katika upataji wa huduma za afya. Uthibitisho Unganifu wa Magonjwa ya Kitoto (IMCI) umeonyesha kuwa na matokeo mazuri katika baadhi ya maeneo ya wilaya. Kwa hiyo, upanuaji wake katika wilaya zote uwe kipaumbele cha kwanza.

Theluthi moja ya watu waliohojiwa ambao hawakutumia huduma za afya walipokuwa wagonjwa walisema ni kutokana na gharama kuwa juu.

Mbali ya huduma za afya kuna mambo mengine yanayoathiri kiwango cha afya. Uboreshaji wa elimu ya wasichana na wanawake unaweza kuleta faida nyingi kwa kipindi kirefu, hususani katika maeneo ya matumizi ya dawa za kuzuia mimba na idadi ya uzazi. Elimu ya afya ya kuwaeleza na kushawishi mabadiliko ya tabia ni moja ya njia nzuri na rahisi ya kuboresha afya, inayoweza kuwa na mchango mkubwa kwa watu. Pia, kuna haja ya kushughulikia matatizo ya kijamii na kiuchumi ya wanawake. Wanawake wana mzigo mzito mno, hata wakati wa ujauzito na kulea watoto. Hili huathiri sana afya za wanawake.

Mwisho, VVU/UKIMWI vinabaki kuwa kigezo kikubwa ambacho kitaamua matarajio ya maendeleo ya Tanzania kwa miaka ijayo. Mikakati na shughuli za upunguzaji wa maambukizo ya VVU na madhara yake kwa waathirika vipewe kipaumbele.



Maji na Usafi

Sehemu hii inaangalia viashirio ambavyo vinapima hali ya maji na usafi nchini Tanzania. Usafi ulikuwa ni eneo jipya la kipaumbele katika ripoti ya mwaka 2003. Majedwali ya hapo chini yanatoa ufupisho wa viashirio ambavyo vilitumika, malengo na kiwango cha kila kiashirio. Baada ya majedwali, kuna muhtasari wa maendeleo ya kupunguza umaskini katika eneo hili la kipaumbele, ikiwa ni pamoja na masuala ya sera na mapendekezo. Taarifa nyingi ni zile zile katika ripoti zote mbili kwani hakukuwa na taarifa mpya zilizopatikana kwa baadhi ya viashirio.

Viashirio vyenye malengo (vya mwaka 2003):

Viashirio	Malengo	Kiwango
Asilimia ya watu wa vijijini wanaotumia maji ya bomba au maji salama kama chanzo chao kikuu cha maji ya kunywa	55% ifikapo 2003 85% ifikapo 2010	• 46% ya watu wa vijijini walitumia maji ya bomba au maji salama mwaka 2000/01

Viashirio visivyo na malengo (vya mwaka 2003):[7]

Viashirio	Malengo	Kiwango
Asilimia ya kaya ambazo zina uwezo wa kuchota maji chini ya dakika 20 (kwenda, kuchota, kurudi)	-	• 64% ya kaya za mijini na 65% ya kaya za vijijini (1999)
Idadi ya taarifa za ugonjwa wa kipindipindu	-	• Takwimu zilizokusanywa na Wizara ya Afya bado hazijapatikana
Asilimia ya watoto chini ya miaka 5 waliokuwa na ugonjwa wa kuhara wiki mbili kabla ya utafiti	-	• 12% ya watoto chini ya miaka 5 waliripotiwa kuwa na ugonjwa wa kuhara wiki mbili kabla ya Utafiti wa Uzazi na Afya ya Mtoto Tanzania (1999)
Badiliko la asilimia katika vifo vilivyosababishwa na ugonjwa wa kuhara kwa watoto wa miaka chini ya 5	-	• Hakuna takwimu za taifa–hata hivyo, vifo vinavyotokana na kuhara kwa watoto chini ya miaka 5 vilipungua katika maeneo mawili ya utafiti (Morogoro na Dar es Salaam)

Hitimisho na Mapendekezo

Taarifa ya mwaka 2002 ilihitimisha kuwa kwa kuzingatia vyanzo vya maji ya kunywa haionyeshi sura halisi ya upataji wa maji ya kunywa wa kaya. Mambo mengine muhimu ni:

- Umbali hadi kwenye vyanzo vya maji
- Muda unaotumiwa kuchota maji
- Kiasi cha maji yaliyopo
- Unafuu wa maji

Matokeo yake, viashirio vipya viliwekwa. Kwa wakati huu, ni taarifa za muda na umbali kwenda kwenye maji tu ndizo zilizopo.

> Jumla ya muda wa kuchota maji - kwenda kwenye chanzo, kusubiri, kuchota maji na kurudi nyumbani - vinatoa sura nzuri ya uchotaji maji wa kaya.

Kulikuwa na kuongezeka kwa hali ya juu katika matumizi ya vyanzo vya maji safi katika miaka ya 1990, hususani katika maeneo ya vijijini. Hata hivyo, malengo ya mwaka 2003 hayakufikiwa, na zaidi ya nusu ya kaya za vijijini bado zinategemea vyanzo vya maji ambavyo si salama. Idadi ya kaya (kote vijijini na mijini) zisizo na maji wakati wa kiangazi ambazo hufuata maji umbali wa chini ya km 1 kutoka

[7] Tafadhali zingatia kuwa malengo yalikwisha wekwa baada ya kuandikwa taarifa hii.

nyumbani zimeongezeka katika miaka ya 1990. Asilimia ya kaya ambazo hutumia dakika 30 au chini ya hapo kuchota maji ilipungua katika kipindi cha mwaka kati ya 1991-1999. Wakati huohuo, kaya ambazo hutumia zaidi ya saa 2 kuchota maji zimeongezeka, hasa katika maeneo ya mijini. Hii ni kwa sababu ya utoaji mdogo wa maji na kukua idadi ya watu mijini. Hii inamaanisha kuwa wanawake na watoto hutumia muda mwingi kutafuta maji.

Maji: Masuala Muhimu

- Kuongezeka kwa matumizi ya vyanzo bora vya maji ya kunywa vijijini
- Asilimia ya kaya za Dar es Salaam zinazotumia vyanzo bora vya maji imepungua
- Karibu 1/2 ya kaya nchini Tanzania bara na zaidi ya 1/2 ya wakazi wa vijijini bado wanapata maji ya kunywa kutoka katika vyanzo ambavyo si salama

Hakuna takwimu za hivi karibuni za mwelekeo wa ugonjwa wa kipindupindu. Matukio ya kuhara kwa watoto yalibadilika kidogo katika miaka ya 1990, na yamekuwa zaidi katika maeneo ya vijijini. Takwimu zilizokusanywa kutoka katika maeneo ya utafiti, hata hivyo, zimeonyesha kuwa kumekuwa na kupungua kwa vifo vinavyotokana na ugonjwa wa kuhara katika kipindi cha miaka ya 1990. Iwapo jambo hili ni la kweli kwa nchi nzima, itakuwa ni maendeleo makubwa katika afya ya mtoto.

Kulikuwa hakuna lengo rasmi na viashirio vya usafi katika mwaka 2003. Taarifa za kaya kuhusu usafi zilikuwa za huduma za choo peke yake. Asilimia ya kaya zilizokuwa na choo ilikuwa kati ya 84% na 89% kutoka mwaka 1988 hadi mwaka 1999, na hakukuwa na mabadiliko ya asilimia ya utumiaji wa choo kwa kaya kati ya mwaka 1991–2000. Taarifa za utumiaji wa huduma za vyoo zinatoa sura isiyo kamili ya masuala ya usafi.



HAKI KAZI PHDR SW 9/6/05 9:22 AM Page 16

Kuathirika na Umaskini

Sehemu hii inaangalia viashirio vinavyoonyesha athari za umaskini, ambako kulikuwa ni eneo jipya la kipaumbele katika taarifa ya mwaka 2003. Jedwali la hapo chini linatoa muhtasari wa viashario vilivyotumiwa na kiwango cha kila kiashirio. Baada ya jedwali, kuna muhtasari wa maendeleo ya kupunguza umaskini katika eneo hili la kipaumbele, pamoja na masuala ya sera na mapendekezo.

Viashirio (vya mwaka 2003):[8]

Viashirio	Malengo	Kiwango
Asilimia ya kaya ambazo hazipati zaidi ya mlo mmoja kwa siku	-	• 1.1.% ya kaya ziliripotiwa kula mlo mmoja kwa siku mwaka 2000/2001, ambacho si kiwango cha juu hata kwa maskini
Asilimia ya watoto yatima	-	• Karibu 10% ya watoto chini ya miaka 15 wamepoteza mmoja wa wazazi wao • Karibu 1% ya watoto wamepoteza wazazi wote wawili
Asilimia za watoto wanaofanya kazi na hawaendi shuleni	-	• Karibu 20% ya watoto wenye umri wa miaka 5-17 walikuwa wanafanya kazi na hawakuwa wakienda shuleni (2000/01)
Asilimia ya watu wazima walioonekana kuwa na magojwa sugu	-	• Hakuna takwimu za hivi karibuni za kiashirio hiki
Wastani wa idadi ya siku ambazo watu wazima waliripotiwa kuwa wagonjwa kiasi cha kutofanya kazi	-	• Hakuna takwimu za hivi karibuni za kiashirio hiki

Hitimisho na Mapendekezo

Umuhimu wa kiashirio hiki unakwamishwa na kukosekana kwa taarifa. Hakuna taarifa za mwelekeo wa viashirio vya kuathirika na umaskini wakati wa utekelezaji wa Mkakati wa kwanza wa Kupunguza Umaskini kati ya mwaka 2000-2003. Mwelekeo wa miaka ya 1990 ni ule tu unaowahusu watoto yatima na idadi yake kuongezeka kwa sababu ya VVU/UKIMWI. Aidha, ni dhahiri kuwa idadi ya yatima itaendelea kuongezeka. Katika eneo la ajira ya watoto, kuna watoto zaidi wanaofanya kazi vijijini na wavulana ni zaidi ya wasichana wanaofanya kazi. Umuhimu wa kushughulikia VVU/UKIMWI na kupunguza athari zake kwa watoto bado ni suala la kupewa kipaumbele.

> "Upangaji wa malengo na upimaji wa kiasi cha kuathirika na umaskini bado ni changamoto katika kukosekana kwa uelewa ulio wazi wa dhana…katika mfumo wa Tanzania."
>
> - Taarifa ya Maendeleo ya Mkakati wa kwanza wa Kupunguza Umaskini 2002

Viashirio hivi vinajumuisha jumla ya masuala mengi yanayotofautiana. Pia haviwakilishi orodha kamili ya kundi maskini, pia havijumuishi sababu zote zinazoleta athari za umaskini kwenye kaya za Watanzania. Kulishughulikia tatizo hili ni muhimu kwa ajili ya kupata

[8] Tafadhali zingatia kuwa malengo yalikwisha wekwa baada ya kuandika taarifa hii.

ufumbuzi sahihi wa umaskini uliokithiri. Tathmini Shirikishi ya Umaskini Tanzania inafafanua kwa kina athari za umaskini na kubainisha mbinu nyingi za ufukara ambazo huwaathiri wakazi. Hii inaonyesha kuwa ufuatiliaji hauna budi kulenga zaidi kwenye sababu za ufukara badala ya kwenye makundi mahsusi ya umaskini uliokithiri. Tathmini Shirikishi ya Umaskini Tanzania itasaidia kuvirekebisha viashirio vya umaskini uliokithiri katika sekta nyingine (mf. afya) na kuanzisha vipya.

Uhusishaji wa Umaskini na Mazingira

Sehemu hii inaangalia viashiria vinavyoonyesha uhusishaji wa umaskini na mazingira, ambalo ni eneo jipya la kipaumbele kwenye ripoti ya mwaka 2003. Jedwali la hapo chini linatoa muhtasari wa kila kiashirio. Baada ya jedwali, kuna muhtasari wa maendeleo ya upunguzaji wa umaskini katika eneo hili la kipaumbele, pamoja na masuala ya sera na mapendekezo.

Viashirio (vya mwaka 2003):[9]

Viashirio	Malengo	Kiwango
Idadi ya Mikataba ya Usimamizi wa Pamoja wa Misitu (JFMA)	-	• Aina moja ya JFMA ni Mkataba wa Usimamizi Shirikishi wa Misitu (PFM) • Karibu wilaya zote zina mkataba mmoja au zaidi wa PFM

[9] Tafadhali zingatia kuwa malengo yalikwisha wekwa baada ya kuandika taarifa hii.

Idadi ya Maeneo ya Usimamiaji wa Wanyamapori (WMA)	-	• Kwa sasa WMA zipo katika wilaya 15 tu zinazofanyiwa majaribio, lakini WMA zaidi zinategemewa kuanzishwa katika siku za usoni
Umbali wa kwenda kutafuta kuni	-	• Umbali kwenda kutafuta kuni umepungua kwa wastani kutoka km 3.2 mwaka 1991/92 hadi km 2.7 mwaka 2000/01
Uwiano wa wakulima wadogo kwa eneo lililopandwa pungufu ya hekta 2 kwa ajili ya mazao makuu	-	• Hakuna taarifa za hivi karibuni zilizopatikana, ingawaje Utafiti wa Kilimo unategemewa kutoa taarifa hii

Hitimisho na Mapendekezo

Viashirio vya idadi ya Mikataba ya Usimamizi wa Pamoja wa Misitu (JFMA) na idadi ya Maeneo ya Usimamiaji wa Wanyamapori (WMA) havitoi taarifa za jinsi mabadiliko katika misitu na utunzaji wa wanyamapori unavyoboresha ustawi wa watu. Ushirikishwaji wa jumuiya katika Maeneo ya Usimamiaji wa Wanyamapori (WMA) bado ni dhaifu. Hatua za kuhamasisha ushiriki wa umma katika WMA lazima zichukuliwe.

Yapo maendeleo kiasi katika suala la umbali anaotembea mtu kwenda kutafuta kuni. Kulikuwa na kupungua kidogo katika maeneo ya vijijini kwa wastani wa umbali kwenda kutafuta kuni na kumeongezeka kwa watu maskini na kupungua kwa wale wasio maskini. Tafiti zijazo zionyeshe tofauti kati ya kukata na kununua kuni.

Changamoto katika uchambuaji wa uhusishaji wa umaskini na mazingira ni uchaguaji wa viashirio bora ambavyo vitatoa taarifa juu ya matokeo ya sera za upunguzaji wa umaskini. Ni katika miaka ya hivi karibuni tu ambapo uhusiano kati ya maendeleo, umaskini na masuala ya mazingira uligunduliwa. Viashirio vya rasilimali muhimu za mazingira zinazohusishwa na umaskini haviwakilishwi vizuri katika orodha hii ya sasa, hasa kwa kilimo. Katika siku chache zijazo, serikali itaandaa utafiti wa uhusishaji wa umaskini na mazingira ambao utasaidia kupata viashirio bora.



HAKI KAZI PHDR SW 9/6/05 9:22 AM Page 19

Utawala

Sehemu hii inaangalia viashirio vinavyoonyesha utawala, eneo ambalo lilikuwa jipya katika ripoti ya mwaka 2003. Jedwali la hapo chini linatoa muhtasari wa viashirio vilivyotumiwa na kiwango cha kila kiashirio. Baada ya jedwali, kuna muhtasari wa maendeleo ya upunguzaji wa umaskini katika eneo hili la kipaumbele, ikiwa ni pamoja na masuala ya sera na mapendekezo.

Viashirio (vya mwaka 2003):[10]

Viashirio	Malengo	Kiwango
Asilimia ya Halmashauri za Wilaya zenye taarifa nzuri za ukaguzi kutoka katika Ofisi ya Ukaguzi ya Taifa	-	• 10% tu ya Halmashauri za Wilaya zenye taarifa bora za ukaguzi katika mwaka 2001
Idadi ya matukio ya rushwa yaliyoripotiwa	-	• Idadi ya matukio yaliyoripotiwa iliongezeka kutoka 13 mwaka 1999 hadi 129 mwaka 2002
Idadi ya waliopatikana na hatia ya rushwa	-	• Kulikuwa na waliopatikana na hatia 12 kati ya kesi 129 zilizokuwepo mwaka 2002
Asilimia ya watumishi waandamizi wanawake	-	• 40% ya watumishi walikuwa wanawake katika mwaka 2003, ambao miongoni mwao ni walimu • Endapo walimu wataondolewa, uwiano wa wanawake ni kiasi cha 1/3
Asilimia ya wanawake miongoni mwa wabunge	-	• Mwaka 2000, 27% ya wabunge walikuwa wanawake (62 kati ya jumla ya viti 231) • Kati ya wabunge 62, wanawake 81% walichaguliwa kwa viti maalum vya wanawake • Wanawake waliochaguliwa kwa kura ni 5% ya viti katika Bunge

Hitimisho na Mapendekezo

Karibu Halmashauri zote za Wilaya zimekaguliwa na ni 10% tu ambazo zilipata ripoti bora za ukaguzi. Karibu 40% ya halmashauri katika mwaka 2001 "hazikuwasilisha vizuri au kutoa hali halisi ya ukweli wa fedha za halmashauri", na hili linasababisha matatizo katika matumizi ya fedha za umma. Kuna ushahidi mdogo wa kupungua kwa mwelekeo huu.

Idadi ya matukio ya rushwa yaliyoripotiwa imeongezeka sana kuanzia mwaka 2000, ingawa idadi ya waliotiwa hatiani bado ni ndogo kwani utaratibu wa mashitaka huchukua muda mrefu. Ucheleweshaji huu unaonekana kuwakatisha tamaa watu katika kutoa taarifa zinazohusu rushwa.

[10] Tafadhali zingatia kuwa malengo yalikwisha wekwa baada ya kuandika taarifa hii.



Kulikuwa na ongezeko dogo la uwakilishi wa wanawake katika utumishi. Kulikuwa na ongezeko kubwa la ushiriki wao bungeni, ingawa bado uwakilishi wao ni mdogo.

Halmashauri nyingi za Wilaya kuwa na ripoti mbaya za ukaguzi wa hesabu ni tatizo. Hili linadhihirisha kuwa fedha za umma hazitumiwi ipasavyo na kaguzi za nyuma hazijaleta maboresho yoyote. Kuna haja ya kuyaendesha mashitaka ya rushwa haraka zaidi kama serikali inataka kuendelea kuaminiwa na umma. Jitihada ndogo za kuongeza ushiriki wa wanawake serikalini zinakatisha tamaa na kuonyesha kuwa mabadiliko makubwa yanahitajika.

Muhtasari wa Kiwango cha Umaskini Tanzania

Umaskini wa Kipato

Ukuaji wa uchumi lazima uwe na faida kwa maskini.

Kulikuwa na kupungua kidogo kwa umaskini hasa vijijini katika kipindi cha miaka ya 1990. Maendeleo katika ukuaji wa uchumi sharti yajenge msingi wa kupunguza umaskini, ingawa katika mwaka 2003 kiwango cha ukuaji kinaweza kuonyesha kupungua kwa sababu ya uhaba wa mvua. Kilimo ni muhimu; matatizo makubwa yanayokikabili ni uwekezaji mdogo na mabadiliko ya bei za mazao. Ukosefu wa ajira katika maeneo ya mijini ni mkubwa, hasa kwa vijana. Kuna haja ya kuhakikisha kwamba uwekezaji katika madini na sekta nyingine unakuwa na faida kwa uchumi mzima. Pia, kuna haja ya kuhamasisha uwekezaji katika mikoa mingine mbali na michache ambayo kwa sasa inapata uwekezaji kutoka nje.

Uwekezaji wa umma katika miundombinu, hasa barabara, uchangie katika kupunguza umaskini. Hata hivyo, barabara nyingi bado ni mbaya na mpango wa ukarabati bado haujafanyika. Kiwango cha jumla cha ukarabati wa barabara ni kidogo, na ubora wa barabara utapotea kutokana na kutotengenezwa mara kwa mara.

HAKI KAZI PHDR SW 9/6/05 9:22 AM Page 21

Uwezo wa Watu, Kuishi na Ustawi

Elimu ya msingi imepata mafanikio makubwa tangu mwaka 2000. Wanafunzi zaidi wanaandikishwa na watoto wanaanza shule ya msingi katika umri mdogo. Hata hivyo, ubora wa elimu inayotolewa bado ni tatizo kubwa, huku kukiwa na idadi ndogo ya wanaofaulu kwenda katika shule za sekondari.

Uwezo wa shule za sekondari umeongezeka, lakini bado hautoshi kuwachukua wanafunzi wote wanaofaulu shule ya msingi. Wasichana wanafanya vibaya sana kwenye mtihani wa kumaliza elimu ya msingi (PSLE) na hakuna uwiano wa kijinsia katika kujiunga na sekondari, na hali hii inaonekana kuendelea kuwa mbaya zaidi. Kuendelea kupanua shule za sekondari kunahitajika, lakini ni lazima ifanywe katika namna ambayo haitazibagua jamii maskini.

Watoto wasiosoma na watu wazima wasiojua kusoma wanasaidiwa kidogo na mfumo wa elimu. Kuna maendeleo madogo katika utoaji wa Mpango wa Elimu ya Msingi kwa Waliokosa (MEMKWA). Malengo ya Mkakati wa kwanza wa Kupunguza Umaskini katika kuondoa ujinga hadi mwaka 2010 hayataweza kufikiwa labda iwapo Mkakati mpya wa Elimu ya Watu Wazima na isiyo Rasmi utatekelezwa kwa makini.

VVU/UKIMWI

- Uambukizaji wa VVU/UKIMWI uliongezeka hadi 9.9% mwaka 2000
- Tofauti kubwa kimikoa za kiwango cha maambukizo ya VVU
- VVU/UKIMWI unabaki kuwa *moja ya masuala makubwa* ambayo yanaamua mustakabali wa kuzama katika maendeleo

Vifo vya watoto wachanga na watoto wengine havikupungua katika kipindi cha miaka ya 1990. Kiwango cha watoto kuugua malaria kilibaki palepale, ingawa taarifa kutoka katika baadhi ya maeneo zilionyesha kupungua kwa vifo vya watoto vilivyosababishwa na malaria. Hakukuwa na mafanikio katika upunguzaji wa utapiamlo kwa watoto katika kipindi cha miaka ya 1990. Idadi ya uzazi ilipungua katika kipindi hicho, lakini bado ni kubwa katika maeneo ya vijijini.



HAKI KAZI PHDR SW 9/6/05 9:22 AM Page 22

Asilimia ya uzazi uliohudumiwa na wauguzi wenye ujuzi na uliofanyika katika vituo vya afya ulipungua kote na pengo kati ya maeneo ya mijini na vijijini liliongezeka. Hata hivyo, kiwango cha matumizi ya dawa za kuzuia mimba na chanjo ya watoto kiliongezeka. Mafanikio katika kiwango cha chanjo kilikuwa zaidi ya malengo ya Mkakati wa kwanza wa Kupunguza Umaskini.

Ubora wa Huduma za Afya

Watu wa vijijini na kaya maskini bado wana ugumu wa kupata huduma bora za afya. Kuna haja kubwa ya kuhakikisha kuwa kila mtu anafikiwa na huduma bora na nafuu. Kwa kuongezea, mikakati na juhudi za kuhamasisha elimu kwa wanawake na kampeni za elimu ya afya ni muhimu. Bila ya kufanya jitihada madhubuti za kupunguza maambukizo ya VVU, idadi ya yatima itaendelea kuongezeka. Hili linabaki kuwa suala la msingi.

Kupatikana kwa Huduma za Afya:

- Pengo kubwa kati ya tajiri na maskini katika upataji wa huduma za afya
- Upataji wa huduma za afya umepungua kwa watu maskini

Kumekuwa na ongezeko kwa kaya kutumia vyanzo salama vya maji vijijini katika miaka ya 1990, lakini hali hiyo sio sawa na mijini. Hata hivyo, zaidi ya nusu ya kaya zote vijijini bado zinatumia maji ya kunywa ambayo si salama, na wanatembea zaidi ya dakika kumi kufikia vyanzo vyao vya maji. Baadhi ya maeneo ya utafiti ilionyesha kupungua kwa vifo vya watoto vilivyotokana na ugonjwa wa kuhara mwishoni mwa miaka ya 1990, lakini kuna ushahidi mdogo wa kupungua huku katika tafiti za taifa za kipindi hicho hicho.

Utawala

Mwelekeo katika utawala unaonyesha sura mchanganyiko. Kumekuwa na kuongezeka kwa kiwango cha ukaguzi wa Halmashauri za Wilaya, lakini hakukuwa na ongezeko la idadi ya Halmashauri zilizotoa taarifa nzuri. Kuna haja kubwa ya kuboresha mahesabu ya fedha za umma katika ngazi hii ya serikali. Kumekuwa na ongezeko la idadi ya matukio ya rushwa yaliyoarifiwa, lakini uendeshaji wa mashitaka ni wa taratibu mno.

Uchelewaji katika uendeshaji wa mashitaka ya rushwa unatokana na uhaba wa maofisa upelelezi. Ili kuwa na wafanyakazi wa kutosha maofisa upelelezi 2,311 wanahitajika.

- **Mapitio ya Matumizi ya Umma 2004**

Jinsia

Pengo la kijinsia linajionyesha katika maeneo mengi (angalia kisanduku). Kwanza kabisa, ni katika elimu, uandikishwaji wa wasichana katika shule ya msingi ni sawa na wa wavulana, lakini kiwango chao cha kufaulu mtihani wa elimu ya msingi ni kidogo. Uandikishwaji wa wasichana katika shule za sekondari pia ni mdogo na unaonekana kuzidi kudorora. Jitihada za kushughulikia nyanja zote za tatizo hili ni lazima zifanywe.

Wanawake na wasichana wanapata taabu nyingi katika maeneo yafuatayo:

- Elimu
- Afya
- Maji
- Serikali

Huduma za afya ambazo ni muhimu katika kupunguza vifo vya watoto wakati wa uzazi ni duni. Kiwango cha ujumla cha idadi ya uzazi bado ni kikubwa na matumizi ya dawa za kuzuia mimba ni madogo.

HAKI KAZI PHDR SW 9/6/05 9:22 AM Page 23

Matatizo ya upataji wa maji, ambayo kwa kawaida huwakabili wanawake na watoto, bado ni makubwa kwa baadhi ya kaya. Moja kati ya kaya kumi za vijijini huchukua zaidi ya saa mbili kuchota maji kwa kichwa, na kiwango hiki kilionekana kuongezeka kwa miaka yote ya 1990.

Ushiriki wa wanawake serikalini pia ulibaki kuwa mdogo. Kumekuwa na ongezeko dogo tu katika uwakilishi wa wanawake katika utumishi. Ingawa kumekuwa na mabadiliko makubwa bungeni, bado uwakilishi wa wanawake ni mdogo.



3. Mada Muhimu za Umaskini

Sehemu hii inashughulikia mada muhimu zinazohusiana na umaskini zilizomo katika Taarifa zote mbili za Umaskini na Maendeleo ya Watu. Mada hizi zinatokana na uchambuzi wa viashirio vya upunguzaji wa umaskini. Mada hizi ni tofauti kwa kila ripoti, ingawa kuna baadhi ya maeneo yanayofanana. Jedwali la hapo chini linaorodhesha mada muhimu zilizoshughulikiwa na kila ripoti.

Taarifa ya Umaskini na Maendeleo ya Watu 2002	Taarifa ya Umaskini na Maendeleo ya Watu 2003
1. Umaskini Mijini	1. Athari za Umaskini na Uangalizi wa Jamii
2. Uhusishaji wa Sera za Jumla na Umaskini	2. Faida Inayotarajiwa (Sekta ya Maji)
3. Athari za Umaskini	3. Utawala
	4. Kilimo

Kama jedwali linavyoonyesha, athari za umaskini zimetolewa katika ripoti zote mbili. Hii inaonyesha umuhimu wake katika kuuelewa umaskini, vyanzo vyake na namna ya kuushughulikia. Sura hii inaonyesha muhtasari wa mada hizi muhimu zinazohusiana na umaskini.

Umaskini Mijini

Kuna kiwango kikubwa cha umaskini katika maeneo ya vijijini nchini Tanzania. Hata hivyo, suala la umaskini mijini pia ni la muhimu. Utafiti wa Bajeti ya Kaya ya mwaka 2000/01 unaonyesha kuwa umaskini katika maeneo ya mijini umepungua katika kipindi cha miaka kumi iliyopita, hususani katika jiji la Dar es Salaam. Hata hivyo, kuna makundi maalum mijini ambayo yamebaki kuwa maskini na yanayoathirika zaidi. Makundi haya yana uwezekano mkubwa wa kuanguka kwenye umaskini. Umuhimu katika maeneo ya mijini lazima uwekwe kwenye makundi yafuatayo:

- Vijana wasio na ajira
- Watu waishio mitaani
- Wafanyabiashara wadogo katika sekta zisizo rasmi ambao wana uwezo mdogo wa kupata kipato
- Watu waishio katika miji yenye miundombinu mibovu ya kijamii
- Watu wanaoishi katika hali ya umaskini na kutengwa

Masuala muhimu matatu yalichunguzwa ili kuuelewa umaskini wa mijini:

1. Sekta isiyo rasmi
2. Hali ya kuishi
3. Upataji wa huduma za jamii

Sekta isiyo Rasmi

Kumekuwa na ongezeko kubwa la idadi ya watu wasio na ajira rasmi mijini. Ukosefu wa ajira ni mkubwa hasa miongoni mwa vijana. Sekta isiyo rasmi imekua sana kutokana na biashara huria mijini na pia kutokana na kiwango cha juu cha ukosefu wa ajira. Sekta isiyo rasmi hasa inajumuisha wafanyabiashara wadogowadogo, ambao mara nyingi ni vijana wenye umri wa kati ya miaka 20 hadi 29. Karibu 92% ya vijana hao wana elimu ya msingi tu na hawana mafunzo yoyote ya ujuzi. Mbali ya biashara ndogondogo, wakazi maskini wa mijini wanajihusisha na kuchekecha mchanga wa madini, kuponda mawe, na utengenezaji wa chokaa kwa ajili ya shughuli za ujenzi zinazokua kila siku. Watu wa

aina zote hushiriki katika shughuli hizi. Wana elimu ya msingi tu, njia mbadala chache, na hutumia zana duni za kazi. Idadi ya watoto wanaoshiriki katika shughuli hizi zisizo rasmi huko mijini imeongezeka.

Hali ya Kuishi

Watu maskini wana uwezo mdogo wa kupata ardhi na nyumba mijini kwa sababu ya gharama ya juu, hivyo hubaki wakiishi kwenye maeneo yasiyopimwa, yaliyotengwa na ya hatari. Katika maeneo haya huduma za jamii ni za duni kwa sababu hakuna miundombinu na fedha za kutosha. Jijini Dar es Salaam watu maskini wengi huishi mabondeni ambako kuna hatari ya mafuriko. Wingi wa watu pia ni tatizo – mara nyingi kunakuwa na zaidi ya familia moja inayoishi katika chumba kimoja. Idadi ya watu wasio na makazi imeongezeka. Inakadariwa kuwa watu 15,000 hadi 20,000 katika jiji la Dar es Salaam wanaishi mitaani, ikiwa ni pamoja na watoto wengi.

Upataji wa Huduma za Jamii

Watoto maskini walioko mijini hawana uwezo wa kupata elimu. Hakuna shule za kutosha, hivyo, madarasa yamejaa wanafunzi, pia vifaa vya elimu ni duni na hakuna walimu wa kutosha. Kaya maskini haziwezi kumudu kununua sare na gharama nyingine za mahitaji ya shule. Kiwango kidogo cha elimu miongoni mwa maskini wa mijini huwafanya wakose nafasi za ajira na kuwa na kipato kidogo. Hili linachangia kwa wao kuwa na makazi duni, lishe duni, kutumia maji yasiyo salama na afya duni. Afya duni husababishwa na ukosefu wa maji safi, utapiamlo na uwezo mdogo wa kupata huduma za afya. Watu maskini hawawezi kumudu kulipia ada inayotozwa na hospitali na zahanati. Magonjwa ya kuambukizwa ni mengi kwa sababu ya uchafu katika baadhi ya maeneo yenye watu wengi jijini Dar es Salaam. Upataji wa maji safi na ya kutumainiwa ni suala kubwa. Idadi ya kaya zinazotumia maji ya bomba jijini Dar es Salaam imepungua katika miaka ya 1990 kwa sababu miundombinu ya maji jijini haitoshelezi idadi ya watu wanaoishi jijini. Jambo hili huwalazimisha watu watumie vyanzo visivyo salama vya maji. Baadhi ya vitongoji visivyopimwa vina upungufu mkubwa wa maji, ambao unachangia kuzuka kwa magonjwa ya mlipuko kama kipindupindu na kuhara. Pia ni mahali ambako wanawake na watoto wanakabiliwa na hali ngumu kufuata na kusubiri maji kwa muda mrefu katika sehemu ambazo ni mbali. Gharama kubwa ya maji pia huwafanya watu maskini washindwe kupata mahitaji mengine muhimu.

Masuala ya Sera

- Shughuli za kupunguza umaskini zilengwe vijijini – hata hivyo, kuna haja ya kuyalenga makundi mahsusi ya maskini na yanayoathirika na umaskini (angalia yale yote yaliyoorodheshwa mwanzoni mwa sehemu hii).

- Kuna idadi kubwa ya vijana ambao hawana ajira mijini. Ni lazima kutafuta nafasi za ajira kwa vijana kote vijijini na mijini. Wana umuhimu mkubwa katika kuchangia kukua kwa uchumi. Pia, ni hatari kuwa na idadi kubwa kama hiyo ya vijana ambao wanajiona kuwa wamesahaulika.

- Sekta isiyo rasmi ni kubwa na inakua mijini. Hata hivyo, sekta isiyo rasmi ina matatizo ya kutokuwa na mazingira salama, yasiyo na uhakika wa maisha endelevu na yenye hatari pamoja na mazingira yasiyoiwezesha jamii kuondokana na umaskini. Kusudi muhimu la upunguzaji wa umaskini mijini lilenge kuondoa vikwazo hivyo kwa ajili ya kuboresha shughuli za sekta isiyo rasmi.



- Miundombinu katika maeneo mengi ya makazi ya mijini ni duni. Maendeleo ya miundombinu hayawiani na idadi ya watu wanaokimbilia mijini. Tatizo jingine ni kuwa hakuna nyumba za kutosha na za gharama nafuu. Hii inamaanisha kuwa kuna wanafamilia wengi wanaoishi katika chumba kimoja. Mgawanyo wa maji pia hautoshi kwa idadi inayoongezeka ya watu, hii husababisha uchafu na hatari za kiafya. Ukosefu wa ushughulikiaji wa takataka na uchafuzi wa hewa pia ni tatizo.

Uhusishaji wa Sera za Jumla na Umaskini

Mageuzi ya kiuchumi tangu katikati ya miaka ya 1980 yamesaidia kukuza na kuimarisha uchumi. Hata hivyo, umaskini wa kipato haujabadilika kwa Watanzania walio wengi. Ni muhimu kulishughulikia pengo hili kati ya ukuaji wa uchumi na upunguzaji umaskini. Sehemu hii inayaangalia masuala mawili:

- Ukuaji wa uchumi unaowajali maskini, unaolenga katika kilimo, utalii na madini
- Uhusishaji wa ngazi ya kitaifa na mamlaka za chini katika huduma za jamii, unaolenga kwenye afya na elimu

Ukuaji wa kilimo ni muhimu katika ukuaji wa uchumi unaowajali maskini na kupunguza umaskini kwani Watanzania walio wengi wanategemea kilimo kwa ajili ya maisha yao. Hata hivyo, sekta ya kilimo inakua polepole, wakati sekta za madini na utalii zinakua haraka katika miaka ya hivi karibuni. Kwa hiyo, ni muhimu

Ukuaji wa uchumi lazima uwajali maskini - maana yake utoe nafasi kwa watu wengi kushiriki katika shughuli za uzalishaji na katika kugawa manufaa.

kuchunguza mchango wa sekta hizi katika kupunguza umaskini. Hili linafanywa kwa kuangalia uhusiano wa sekta za madini na utalii pamoja na sekta nyingine na namna uhusiano huu unavyoweza kuwasaidia watu maskini.

Uhusishaji huo unaweza kuboreshwa na sera za serikali. Kwa mfano, Mkakati wa kwanza wa Kupunguza Umaskini umebainisha sekta muhimu za jamii ambazo zitapokea fedha zaidi ili kusaidia kupunguza umaskini. Sehemu hii itaangalia sekta za afya na elimu, hususani utoaji wa huduma za afya ya msingi na elimu ya msingi.

Ukuaji wa Uchumi Unaowajali Maskini

Kilimo

Kilimo bado ni tegemeo kubwa la maisha ya Watanzania wengi. Hivyo, ukuaji wa kilimo utasaidia katika uboreshaji wa kiwango cha maisha ya watu. Urekebishaji wa uchumi una mchango katika kilimo. Biashara huria na uondoaji wa ruzuku una athari zifuatazo:

- Kuongezeka kwa bei za pembejeo
- Kuongezeka kwa riba za mikopo
- Bei ndogo ya mazao, ambayo mara nyingi hupangwa na walengwa
- Vyama vya ushirika sio wanunuzi na wauzaji wa pembejeo peke yao tena

Ingawa kulikuwa na baadhi ya matatizo katika kilimo, mageuzi yake yamefanya mazingira yawezeshe uwekezaji binafsi katika sekta hiyo. Hata hivyo mageuzi haya yanategemewa kuleta ukuaji endelevu wa kilimo kwa kipindi kirefu.

Sekta ya kilimo imeendelea kukua kwa zaidi ya 3% ndani ya kipindi cha miaka kumi iliyopita. Ukuaji huo umekuwa na sawa na nyanja zingine zilizobaki za uchumi. Hii ina maana kuwa mchango wake katika Pato la Taifa wa 50% haujapungua. Hata hivyo, ukuaji huu hautoshi kupunguza umaskini wa vijijini. Ili kupunguza umaskini vijijini kilimo ni lazima kikue kwa haraka zaidi.

Kuna sababu nyingi za kwanini mageuzi ya uchumi mkubwa hayaboreshi ukuaji wa kilimo na kupunguza umaskini vijijini.

• Utegemeaji wa jembe la mkono na kilimo kinachotegemea mvua za msimu kwa wakulima wadogo • Vichocheo vidogo katika kilimo havijasaidia katika ukuaji au uwekezaji – wakulima wanapata faida ndogo na kulipa kodi nyingi • Ukosefu wa masoko ya ushindani • Gharama kubwa za usafiri • Ukosefu wa mikopo kwa wakulima	• Tatizo la upataji wa pembejeo • Uhamasishaji mdogo wa kutumia maarifa kutoka katika utafiti kwenda katika matumizi • Udhaifu katika usambazaji wa huduma za kilimo • Miundombinu mibovu vijijini • Kukosekana kwa taarifa zinazohusu bei • Kukosekana kwa chombo cha wakulima wadogo na chenye nguvu ambacho kingewasaidia wakulima wadogo kuelezea vipaumbele na kudai mahitaji yao

Gharama inayotumiwa na serikali katika kilimo inaweza kuwa na mchango mkubwa kama italenga kwenye maeneo sahihi. Utafiti uliofanywa nchini India unaonyesha kuwa serikali kutumia gharama katika barabara na utafiti na maendeleo kumesaidia kuinua pato la vijijini na kuongeza ukuaji katika uzalishaji. Utafiti mwingine wa nchini Tanzania uliofanywa mwaka 1999 umeonyesha kuwa wakazi wenye kipato kidogo na wakulima wa vijijini hufaidika zaidi kutokana na miundombinu bora. Kugharamia elimu pia kuliathiri ukuaji wa uchumi na uondoaji wa umaskini.

Utalii

Shughuli za utalii zipo zaidi katika maeneo ya Hifadhi za Wanyamapori za Kanda ya Kaskazini, Dar es Salaam, na Zanzibar. Udhibiti wa serikali katika utalii ulikuwa wa juu hadi mwanzoni mwa miaka ya 1990, wakati mageuzi makubwa yaliporuhusu kampuni binafsi. Pato la utalii lilikua kutoka 6% kati ya mwaka 1993-98 hadi 12.4% mwaka 1999. Kulingana na utafiti uliofanywa mwaka 2001, utalii una faida kubwa kwa vile unategemea sekta nyingine kwa bidhaa nyingi na huduma. Hata hivyo, taarifa hizi zinaashiria thamani ya utalii na sio utalii unachangia nini katika uchumi wa Tanzania. Ili kuuhusisha utalii na uchumi wa ndani ni muhimu kuiwezesha jamii na kaya maskini kushiriki kikamilifu kwa kuuza bidhaa na kutoa huduma.

Madini

Sekta ya madini inakua haraka, hasa kwa sababu ya sera za serikali zinazoboresha maendeleo yake. Kiwango hiki cha ukuaji kinaonyesha kuwa katika siku za usoni madini yatakuwa na mchango mkubwa katika uchumi, hasa katika usafirishwaji nje. Kuna sekta mbili ndogo katika madini ambazo zinahusu uwekezaji wa kigeni (migodi mikubwa) na uchimbaji mdogo. Kuna kiasi cha wachimbaji wadogo 100,000 wanaofanya kazi katika migodi midogo. Migodi hii midogo inakabiliwa na matatizo mengi, ikiwa ni pamoja na ajira ya watoto, faida isiyo na uhakika na utumiaji wa mbinu duni na wakati mwingine za hatari za uchimbaji wa madini. Uhusiano wa kiuchumi kati ya madini na uchumi mwingine ni mdogo.

Uchimbaji mdogo umechangia pato dogo la kodi, ingawaje inaongeza pato la nje. Faida ya ajira inakwamishwa na uwezo mdogo na ujuzi mdogo kwenye ngazi za vijijini. Ili kuboresha uhusishaji kati ya migodi mikubwa na migodi midogo, ujuzi wa ndani lazima uendelezwe. Kuwepo kwa shughuli za kiuchumi na huduma za jamii kwenye maeneo yanayozunguka migodi ni muhimu katika kuhusisha madini na upunguzaji wa umaskini. Pia, kampuni chache za madini zinachangia katika elimu na huduma za afya kwa watumishi wao.



HAKI KAZI PHDR SW 9/6/05 9:22 AM Page 29

Uhusishaji wa Ngazi ya Kitaifa na Mamlaka za Chini katika Huduma za Jamii

Uhusishaji wa ngazi ya kitaifa na mamlaka za chini upo bayana hasa katika sekta za afya na elimu kwa sababu serikali imeweka kipaumbele katika uboreshaji wa upataji wa elimu bora ya msingi na huduma za afya ya msingi.

Afya

Kwa kulinganisha na nchi za jirani, Tanzania imekuwa inafanya vizuri sana katika kutoa kipaumbele kwenye kugharamia afya. Hata hivyo, taarifa kutoka katika viashirio vya afya vinaonyesha kuwa kulikuwa na ubora mdogo sana wa utoaji wa huduma za afya na hali ya afya ya watu. Kuna sababu nne ambazo zingeweza kuelezea kwa nini tatizo hili linatokea:

1. Kiwango cha ugharamiaji kinachotakiwa kuboresha afya nchini Tanzania ni kikubwa sana kiasi cha kuongeza gharama ya matumizi ya umma haitoshi.
2. Matumizi ya jumla yanatosha lakini yanatumiwa katika vipaumbele visivyotakiwa.
3. Matumizi ya jumla yanatosha na yanatumiwa katika vipaumbele halisi, lakini kuna upungufu ambao unapunguza mchango wake katika maisha ya watu.
4. Mwisho, inaweza kuwa kwamba sababu hizi zote (1-3) zinatokea kwa wakati mmoja.

Kila moja ya sababu hizi inachambuliwa katika sehemu hii. Jedwali la hapo chini linatoa muhtasari wa uchambuzi.

Sababu	Maelezo
Kiwango cha ugharamiaji kinachotakiwa kuboresha afya nchini Tanzania ni kikubwa sana kiasi kwamba kinachoongezeka katika gharama ya matumizi ya umma hakitoshi.	Kwa sababu ya magonjwa mbalimbali nchini Tanzania (mf. malaria, VVU/UKIMWI, n.k.), kiasi cha fedha kinachotumiwa katika huduma za afya hakitoshi kusaidia viashirio vya afya. Kwa sasa hivi, serikali inatumia dola za kimarekani 6 kwa mtu katika afya, hata hivyo, kiasi kinachohitajika ni dola za kimarekani 12. Kwa vile ongezeko la ugharamiaji katika afya limeshindwa kuleta mchango, ni vizuri kupanga upya vipaumbele ili fedha zitumike katika namna bora zaidi.
Matumizi ya jumla yanatosha lakini yanatumiwa katika vipaumbele visivyotakiwa.	Bajeti inayopangwa kwa ajili ya sekta ya afya itawasaidia maskini kama fedha zitapelekwa kwenye vituo vya huduma ya afya wilayani ambavyo hutumiwa na maskini, huduma ya afya ya kujikinga, na usambazaji wa dawa muhimu. Uchambuzi wa gharama za sekta ya afya katika mwaka 1994/95 unaonyesha kuwa mgawanyo ulikuwa mbaya. Hii ni kwa sababu hospitali za rufaa, hospitali za mkoa/wilaya, vituo vya afya na zahanati vyote vilipokea kiasi sawa cha fedha. Hata hivyo, hospitali za wilaya, vituo vya afya, na zahanati vinatumiwa na 55% ya watu maskini hivyo vingepokea fedha zaidi. Kwa upande mwingine, kumekuwa na ongezeko la jumla la gharama za huduma za afya za wilaya tangu mwishoni mwa miaka ya 1990. Pia, gharama ya usambazaji wa dawa imeongezeka sana katika kipindi cha miaka kumi iliyopita.

Matumizi ya jumla yanatosha na yanatumiwa katika vipaumbele halisi, lakini kuna upungufu.	Utafiti uliofanywa mwaka 2001 unaonyesha kuwa kuna upungufu wa fedha za "gharama nyinginezo" (mf. usambazaji wa dawa) katika kiwango cha wilaya. Hii ni kwa sababu Halmashauri za Wilaya zilitenga fedha kwenye shughuli zaidi ya zile zinazotoa huduma za afya ya jamii. Pia hakukuwa na uwazi kuhusiana na mgawanyo wa fedha. Hii ni kwa vile zahanati/vituo vya afya huwa mara zote haviambiwi juu ya utoaji wa fedha na mgawanyo wake. Yote haya hupunguza kiasi cha fedha kilichotumika kwa ajili ya huduma za afya.
Sababu zote tatu za juu hutokea kwa wakati mmoja.	Inawezekana kuwa sababu zote hapo juu zinaelezea kwa nini kuna udhaifu katika kuhusisha mtazamo wa ngazi ya kitaifa na mamlaka za chini katika Sekta ya Afya – hii ina maana kuwa kuna pengo kati ya matumizi ya sekta ya afya na uboreshaji wa kiwango cha huduma za afya.

Elimu

Katika miaka michache iliyopita, serikali imeongeza bajeti yake ya kawaida kwa sekta ya elimu. Sekta ya elimu inapokea fedha zaidi kati ya zile zote za sekta za vipaumbele. Katika sekta ya elimu, elimu ya msingi inapokea fedha zaidi, ambazo zinawasaidia watu wengi ikiwa ni pamoja na maskini. Hii inaonyesha kuwa mgawanyo kwenda kwenye sekta ya elimu unaelekea zaidi kuwasaidia maskini.

Mgawanyo wa bajeti kwenye "gharama nyinginezo" - kama vile zana za kufundishia na kujifunza - hazijawahi kutosha. Matatizo haya yanaathiri ubora wa elimu, hasa kwa familia maskini ambazo haziwezi kumudu mahitaji ya shule ya watoto wao. Kwa upande mwingine, mgawanyo huu umeongezeka kutoka dola 2 kwa mwanafunzi mwaka 1998/99 hadi dola 8 katika mwaka 2001/02. Hata hivyo, kila mwanafunzi anapokea dola 1 tu kulingana na taarifa zilizopatikana katika ngazi za chini. Taarifa mbalimbali kutoka serikalini na utumishi zinaonyesha kuwa mamlaka za umma mara zote hazionyeshi matumizi ya fedha za elimu. Matokeo yake, serikali imeagiza kuwa mgawanyo wa elimu katika ngazi ya vijijini uchapwe gazetini kuongeza uwazi na uwajibikaji. Japokuwa huu ni mwanzo mzuri, ni vizuri pia kuongeza ufahamu wa umma kuwa taarifa hizi zimo magazetini.

Utafiti wa mwaka 2001 ulionyesha kuwa elimu imegharimiwa kidogo kutokana na sababu zifuatazo:

- Fedha zinazoingia kwenye Halmashauri za Wilaya hazitabiriki, kwa kiasi na wakati – hili husababisha matumizi mabaya ya fedha hizo
- Kuna ucheleweshaji mkubwa katika utoaji wa fedha, hasa zile za "gharama nyinginezo", ambalo ni tatizo hasa katika maeneo ya vijijini
- Fedha za elimu mara nyingi hutumiwa tena kwenye maeneo mengine
- Hakuna utaratibu mzuri wa usimamizi katika kiwango cha serikali kuu wa utoaji na utumiaji wa fedha za elimu na Halmashauri za Wilaya

Masuala ya fedha yana athari kubwa kwenye idadi na ubora wa walimu, ambavyo huathiri ubora wa elimu ya msingi. Idadi ya walimu imeshuka na idadi ya wanafunzi imeongezeka tangu mwishoni mwa miaka ya 1990, ambayo inamaanisha kuwa ukubwa wa madarasa umeongezeka. Uwezo wa walimu pia unaathiri ubora wa elimu. Kulingana na ripoti ya sekta ya elimu ya mwaka 2000 ni 0.5% tu ya walimu wenye diploma. Walimu walio wengi wana ama daraja la IIIA au B/C. Masuala haya huathiri kufaulu kwa wanafunzi katika mtihani wa elimu ya msingi, ambayo ni dhaifu, kwani asilimia kubwa ya wanafunzi hawafikii alama inayotakiwa ili kufaulu.

HAKI KAZI PHDR SW 9/6/05 9:22 AM Page 31

Athari za Umaskini na Uangalizi wa Jamii

Athari za umaskini ni hatari kwa mtu, kaya au jamii inayokabiliwa na kupungua kwa ustawi wao. Kwa maneno mengine, athari za umaskini zinahusu uwezekano wa watu kuwa maskini zaidi kesho kuliko walivyo leo. Kinachoonyesha athari za umaskini ni kiwango cha rasilimali zilizopo ambazo mtu anazo. Kwa hiyo hili ni eneo muhimu la sera na utekelezaji wa upunguzaji wa umaskini, kwani linapanua sera za kupambana na nguvu za umaskini.

Sababu Zinazoleta Umaskini

Zipo sababu kadhaa ambazo zikitokea, huongeza uwezekano wa mtu kuwa maskini. Kuwa fukara kunaweza kusababishwa na matukio ya ghafla, yasiyotegemewa au msukumo uliopo. Mtu hutegemea rasilimali au mfumo unaosaidia kupunguza athari za hali kama hiyo. Hatari za kuwa maskini zipo mara zote, lakini ili kuondokana na ufukara nguvu za umaskini lazima ziwe kubwa kuliko uwezo wa mtu wa kuzipunguza. Baadhi ya sababu za umaskini hazitabiriki na baadhi zinajulikana na zinaendelea. Kuna aina sita za sababu za umaskini:-

1. Marekebisho ya uchumi
2. Mazingira
3. Utawala
4. Sababu za kijamii na kimila na desturi
5. Hali ya afya
6. Hatua za maisha

Makundi Yanayoathirika Zaidi

Watu binafsi, kaya, au jamii zinazokabiliwa na hatari na uwezo mdogo wa kuondokana na umaskini ndizo zinafikiriwa kuathirika zaidi. Matokeo kutoka Tathmini Shirikishi ya Umaskini Tanzania (TzPPA) yanaonyesha makundi makuu 7 yanayoathirika zaidi nchini Tanzania. Makundi haya ni:-

- Watoto
- Walemavu
- Vijana
- Wazee
- Wanawake
- Watumiaji wa dawa za kulevya na walevi
- Watu wanaoishi na magonjwa ya muda mrefu au VVU/UKIMWI

Mwelekeo wa Programu za Uangalizi wa Jamii

Watafiti wamepitia programu kadhaa za uangalizi wa jamii zinazotekelezwa na watu binafsi, kaya, jumuiya, serikali na asasi zisizo za serikali (NGOs). Programu hizi zinajumuisha jitihada za kuzuia athari za umaskini na umaskini wenyewe. Baadhi ya programu za uangalizi wa jamii zinayashughulikia makundi mengi, wakati mwingine zinalenga kwenye kundi moja la maskini. Taarifa za hapa hazitoi tathmini nzima ya programu zote, bali zinaonyesha utendaji wa mashirika katika ngazi ya taifa. Orodha ifuatayo inaonyesha baadhi ya masuala muhimu:-

- Sehemu muhimu za programu hizi zinalenga katika utawala na nguvu za kiuchumi zinazosababisha athari za umaskini
- Programu hizi mara nyingi hazishughulikii umaskini unaosababishwa na mazingira, mila na desturi, afya, na hatua za maisha

- Programu zinazoshughulikia moja kwa moja masuala mahsusi, mf. upataji wa mikopo kwa maskini, kwa kawaida huzifikia wilaya chache tu
- Hakuna programu ambazo zilionyesha kwa urahisi kadirio la idadi ya watu wanaonufaika
- Vyanzo vikuu vya fedha ni serikali na wafadhili wa kimataifa, hivyo uendeleaji wa programu hutegemea kuwepo kwa fedha za kutoka nje
- Idara nyingi za wilaya na asasi zisizo za serikali ni watekelezaji wakuu wa programu nyingi

Mapendekezo kwa Makundi Mahsusi yaliyo katika Hatari ya Kuathirika na Umaskini

Yafuatayo ni baadhi ya mapendekezo ya kushughulikia mahitaji ya makundi mahsusi yaliyo katika hatari ya kuathirika na umaskini. Yamechukuliwa kutoka katika uchambuzi wa mwelekeo wa programu za uangalizi wa jamii. Mapendekezo hayo yamefupishwa katika jedwali la hapo chini:

Makundi Yanayoathirika Zaidi na Umaskini	Mapendekezo
Watoto	• Rasilimali zaidi za serikali zitolewe kwa ajili ya uangalizi wa watoto. Asasi zisizo za kiserikali zisambaze na kuendeleza uwezo huu. • Utekelezaji wa sheria na sera zilizopo zinazohusiana na watoto. • Kuongeza jitihada za kutoa elimu kwa watoto waliopita umri wa kwenda shule kupitia Mkakati wa Elimu ya Msingi kwa Waliokosa (MEMKWA) na Vituo vya Elimu ya Ufundi (VETA). • Kuweka mazingira mazuri ya kusoma ili kuzuia wanaokatiza masomo.
Wanawake	• Kusambaza programu za kuwapa uwezo ili kuongeza uwezo wao wa kumiliki rasilimali. • Kusambaza mifumo ya ushauri wa raia kama vile taasisi za kisheria hasa kwa wanawake maskini ili kuwawezesha kupata haki zao. • Kusambaza programu za ufahamu wa jamii na usambazaji zaidi wa taarifa juu ya afya ya msingi ya uzazi/mtoto, usafi, na kujikinga dhidi ya VVU/UKIMWI. • Kuongeza upataji wa mikopo kwa wanawake maskini. • Kuongeza ufahamu na kuhamasisha utekelezaji wa sheria mpya inayowalinda wanawake, mf. Sheria ya Makosa ya Kujamiiana. • Kuwawezesha wasichana na wanawake kupata elimu ya juu.
Walemavu	• Kusambaza mifumo ya utetezi ambayo inawasaidia walemavu kupata haki zao, huduma muhimu na rasilimali. • Kuendesha kampeni za kuamsha ufahamu wa umma ili kujumuisha haki za walemavu katika maendeleo ya jamii. • Kusambaza mikopo kwa walemavu. • Kuongeza nafasi za masomo ya elimu ya ufundi kwa walemavu. • Kuunda nyenzo zaidi zinazoweza kutumiwa na walemavu. • Kusambaza kwenye nchi nzima mfumo wa uangalizi wa jamii.

Wazee	• Kuwasamehe wazee katika uchangiaji wa gharama za afya na huduma nyingine za msingi ili kuwawezesha kuzipata. • Kuanzisha mfumo wa uhifadhi wa jamii unaofaa katika hali ya uchumi-jamii ya Tanzania ambao utasaidia kuwatunza wazee.
Wagonjwa wa muda mrefu	• Kusambaza programu za kuwasaidia wagonjwa wa muda mrefu, hususani kupitia huduma za afya za majumbani. • Kusambaza programu ambazo zitajenga uwezo wa taasisi kuzisaidia familia kuwatunza wagonjwa wa muda mrefu.
Watumiaji wa dawa za kulevya na walevi	• Kusambaza programu za kuwasaidia watumiaji dawa/pombe kuacha na kuwaganga vijana walioathirika katika maeneo ya nje ya Dar es Salaam, hasa katika miji midogo. • Kuongeza shughuli za kukuza ufahamu miongoni mwa watoto wenye umri wa kwenda shule juu ya athari za utumiaji wa dawa.
Vijana	• Kuwezesha mafunzo ya vijana na kuboresha uwezo wao wa kupata rasilimali ili wajiingize katika shughuli za uzalishaji. • Kuongeza jitihada za kuhamasisha ushiriki wa vijana katika kufanya maamuzi. • Kuendesha kampeni za kukuza ufahamu ili kubadili fikra na mienendo juu ya majukumu na haki za watoto na vijana. • Kuendeleza mifumo mizuri ya kifedha ili kuwasaidia watoto maskini ambao hawawezi kuendelea na shule kwa sababu ya gharama.

Mapendekezo ya Jumla

Serikali ichunguze programu za uangalizi wa jamii na kusambaza zile zote ambazo ni za gharama nafuu na zinazosaidia kupunguza idadi ya watu maskini.

Programu zinazoshughulikia sababu nyingi zinazoathiri umaskini zinafanya kazi zaidi kuliko zile zinazolenga sababu moja ya umaskini. Kwa programu za utetezi, watakaonufaika ni muhimu waambiwe juu ya msaada ambao upo na wapi na jinsi gani ya kuupata.

Sera Bora ya Uangalizi wa Jamii inahitajika ili:

- Kurahisisha utekelezaji wa programu za uangalizi wa jamii
- Kuongeza ukubwa wa programu bora zaidi
- Kuboresha usimamizi wa pamoja na tathmini
- Kubainisha mapengo katika kushughulikia mahitaji ya makundi maskini zaidi

Utaratibu wa wazi wa utoaji wa taarifa uandaliwe ili serikali, wafadhili, na asasi zisizo za serikali zifahamu kiwango cha utoaji wa fedha kwa ajili ya shughuli za uangalizi wa jamii. Serikali pia ihusishwe juu ya utoaji wa fedha za kusaidia uratibu wa programu ili kuongeza ushughulikiaji na matokeo. Ni muhimu kuwa Halmashauri za Wilaya zishirikiane na mashirika ya kijamii, jumuiya, na asasi zisizo za serikali. Hii inamaanisha inahitajika mifumo ya upangaji wa pamoja na utekelezaji wa programu.

Programu nyingi zina muda maalum kulingana na upatikanaji wa fedha za uendeshaji. Programu zilizofanikiwa huongezewa muda na kuhakikishiwa kupewa fedha. Programu ziongeze jitihada zao za kuwa na takwimu sahihi za walionufaika. Pia, washirikiane kupata idadi ya makundi mangapi yanayohitaji msaada wao ili kuboresha programu ya tathmini na matokeo.

HAKI KAZI PHDR SW 9/6/05 9:22 AM Page 34



Faida Inayotarajiwa

Uchunguzi kuhusu faida inayotarajiwa unaangalia tofauti za athari zinazotokana na kaya katika viwango mbalimbali vya uchumi. Kiufasaha zaidi, inamaanisha kutafuta nani anayefaidika kutokana na matumizi ya umma. Utafiti wa sekta ya maji ulifanywa ili kuchambua faida inayotarajiwa.

Utangulizi

Sehemu hii inaelezea njia ambazo Tanzania na wabia wa maendeleo wanazo katika kuitikia malengo ya upunguzaji wa umaskini kwa usambazaji wa maji vijijini. Inaelezea namna ambavyo rasilimali zingeweza kuhamishwa ili kuwa na mchango katika malengo ya Mkakati wa kwanza wa Kupunguza Umaskini ya usambazaji wa maji vijijini, lakini kama tu bajeti zingeweza kubadilishwa zaidi. Kwa sasa, bajeti ya sekta ya maji inaongozwa na mtazamo wa mradi ambapo fedha huenda katika mradi mmoja unaofadhiliwa na mfadhili mmoja. Hii huleta ugumu kwa idara ya mipango katika Wizara ya Maji na Maendeleo ya Mifugo kuitazama upya bajeti kwa kuzingatia upunguzaji wa umaskini. Mfano mahsusi uliotolewa kwa ajili ya kufikia malengo ya Mkakati wa kwanza wa Kupunguza Umaskini katika sekta ya maji ni kuhamisha rasilimali kutoka katika usambazaji wa maji ya bomba kwenda katika usambazaji wa maji yanayotunzwa.

Uchambuzi zaidi wa Upunguzaji Umaskini Unaohitajika

Kuna haja kubwa ya kuelewa faida za kuwekeza katika aina mbalimbali za miundombinu ya maji na usafi. Utafiti uliwasilishwa katika sehemu hii ni jaribio la kuelewa vizuri faida za kuwekeza katika aina mbili za usambazaji wa maji vijijini – maji ya bomba na maji yanayotunzwa. Hili hufanyika kwa kufananisha kiasi cha gharama za umma ambazo huenda kwa watumiaji wa aina mbili tofauti za usambazaji wa maji. Kwa maneno mengine, nani anayetumia maji ya bomba na nani anayetumia vyanzo vya maji vinavyotunzwa?

Usambazaji wa maji ya bomba na yanayotunzwa ni nini?

Vyanzo vya maji ya bomba na yanayotunzwa ni "vyanzo vilivyoboreshwa" kwa vile ni vigumu kwa maji hayo kuchafuka (ukilinganisha na vyanzo visivyotunzwa).

- "Vyanzo vya bomba" ni maji yoyote yanayotoka bombani
- "Vyanzo vinavyotunzwa" hujumuisha visima au chemchemi ambazo huangaliwa kwa kuzungushia vyanzo vya maji ili kukinga uchafu

Matumizi ya Vyanzo vya Maji kwa Kiwango cha Kipato cha Kaya

Kuna uhusiano mkubwa kati ya kipato cha kaya na matumizi ya vyanzo vya maji ya bomba. Kaya tajiri hutumia zaidi maji ya bomba zaidi ya kaya maskini. Kaya za vipato vya viwango vyote hutumia maji yanayotunzwa. Taarifa hizi zinaonyesha kuwa uwekezaji kwenye vyanzo vinavyolindwa umesambazwa sawa zaidi kuliko uwekezaji wa vyanzo vya bomba.

45.9% ya kaya za vijijini Tanzania bara wana uwezo wa kupata vyanzo bora vya maji; 28.3% wanaweza kupata maji ya bomba na 17.6% wanaweza kupata vyanzo vinavyotunzwa.

- Utafiti wa Bajeti ya Kaya 2000/01

Kwa vile kaya nyingi bado zinatumia vyanzo visivyotunzwa, sekta ya maji inahitaji kubainisha njia rahisi na endelevu ya kupunguza idadi ya kaya zinazotumia vyanzo hivi.

Kwanini Kuna Tofauti ya Matumizi ya Maji kati ya Kaya Tajiri na Maskini?

Maji ya bomba yana gharama mara 20 zaidi ya maji kutoka vyanzo vinavyotunzwa, hii inadhihirisha kuwa kaya maskini haziwezi kumudu maji ya bomba (angalia kisanduku). Hata hivyo, vyanzo vya bomba na vinavyotunzwa mara nyingi havipatikani katika kijiji kimoja. Kwa hiyo watu wa vijijini hawana uchaguzi katika kutumia vyanzo vya bomba au vinavyotunzwa. Kwa kawaida, uchaguzi mwingine ni kutumia vyanzo vya asili, kama vile visima vya wazi na mito. Kwa maneno mengine, maamuzi kuhusu chanzo cha maji huamuliwa na maofisa wa mipango na mwekezaji zaidi kuliko mtumiaji.

Ulinganishaji wa gharama ya uwekezaji kwenye vyanzo vya maji ya bomba na yanayotunzwa:

- Gharama ya uwekezaji kwa maji ya bomba ni mara 10-20 zaidi ya gharama ya vyanzo vinavyotunzwa
- Gharama ya uwekezaji kwa muundo mchanganyiko wa bomba na wa kutunzwa ni pungufu mara 4 ya gharama ya maji ya bomba peke yake

Uzoefu wa Shirika la "WaterAid" Tanzania

Kulingana na uzoefu wa shirika la "WaterAid", gharama ya uwekezaji wa bomba ni kiasi cha mara mbili ya kile cha uwekezaji wa maji yanayotunzwa. Hii ni kwa sababu mipango ya maji ya bomba inayogharamiwa na WaterAid kwa kawaida ni kwa kijiji kimoja na inatumia kisima kirefu kimoja, pampu-na-injini, na bomba chache za jamii. Pampu na injini ndiyo vinavyoamua ni muda gani mpango huu utadumu. Ingawa uwekezaji halisi wa mpango wa bomba ni mara 2 tu ya ule wa maji yanayotunzwa, gharama ya vifaa vya ukarabati huzidi kwa 5. Hii inamaanisha kuwa ukarabati wa mpango wa bomba huigharimu bajeti ya serikali zaidi.



Hitimisho

Uwekezaji wa ziada na gharama ya ubadilishaji wa mfumo wa maji ya bomba unasaidia kwa kiasi kikubwa kuzifikia kaya zilizo tajiri za vijijini, kwa vile usambazaji wa maji ya bomba si sawa. Uwekezaji huu unatumia ruzuku ambazo zingetumika kwa manufaa zaidi katika kutunza vyanzo vya asili au kuendeleza vyanzo vya kutunzwa. Inakadiriwa kuwa kila mtu mmoja anayeunganishiwa na maji ya bomba ana gharama ambayo ingewasaidia watu kumi wanaotumia maji yanayotunzwa.

Uwekezaji wa baadaye katika sekta ya maji utambue umuhimu wa usambazaji wa maji katika vyanzo vinavyotunzwa na kuhimiza mchanganyo kati ya bomba na utumiaji wa vyanzo.

Kwa watu maskini, uchambuzi huu hautasaidia kama mpango wa sasa na utaratibu wa bajeti katika sekta ya maji hautarekebishwa. Kuna haja ya kuwa na mabadiliko ya kufanya maamuzi ya ufadhili wa miradi ya maji nje ya mpango rasmi. Utaratibu wa mpango rasmi pia unahitaji kurekebishwa zaidi ili kuendana na malengo ya upunguzaji wa umaskini.

HAKI KAZI PHDR SW 9/6/05 9:22 AM Page 37

Masuala ya Utawala Yanayoathiri Umaskini na Athari Zake

Utawala una mchango mkubwa katika kupunguza umaskini ambao unajumuishwa kwenye Mkakati wa kwanza wa Kupunguza Umaskini. Viashirio vya utawala vilivyoelezwa mwanzoni mwa taarifa hii havitoi taarifa za kutosha, hivyo utafiti mwingine ulifanywa kwenye utawala na upunguzaji wa umaskini. Sehemu hii inabainisha vipengele vya utawala ambavyo huchangia katika upunguzaji wa umaskini na athari zake. Malengo ni katika maeneo makubwa matatu:-

1. Usimamizi wa rasilimali za serikali na uendeshaji wa ofisi za umma
2. Utekelezaji wa sheria na utawala wa sheria
3. Kuelekea katika demokrasia na ushiriki

1. Usimamizi wa Rasilimali za Serikali na Uendeshaji wa Ofisi za Umma

Sehemu hii inaangalia masuala mawili: 1) namna uwajibikaji na uadilifu ulivyo katika ofisi za umma unavyochangia kupunguza umaskini; 2) namna rushwa inavyoathiri utekelezaji wa sera za serikali na mgawanyo wa rasilimali kwa ajili ya upunguzaji wa umaskini na athari zake.

Utaratibu wa Bajeti na Matumizi ya Sekta za Kipaumbele za Kupunguza Umaskini

Utaratibu wa bajeti ni moja ya nyenzo kuu zinazotumiwa na serikali kupunguza umaskini. Serikali sasa ina Muundo wa Matumizi ya Muda wa Kati (MTEF) na Mapitio ya Matumizi ya Umma (PER) kuchunguza kama mgawanyo wa rasilimali unaendana na vipaumbele vya upunguzaji wa umaskini. Bajeti za vijijini zinachapwa magazetini, jambo ambalo huimarisha uwazi. Hata hivyo, umma kwa kiasi kidogo sana hushiriki katika maandalizi ya bajeti.

Kumekuwepo na maendeleo kadhaa katika utoaji wa huduma za jamii kama matokeo ya ongezeko la mgawanyo wa bajeti kwenye sekta za vipaumbele. Hata hivyo, marekebisho ya kuboresha uwazi na uwajibikaji haujaendeleza usimamizi wa fedha kwenye kiwango cha vijijini. Hii inamaanisha kuwa huduma za jamii kwa maskini hazitoshi kwa sababu fedha hazigawanywi vizuri na maofisa wa serikali hawawajibiki.

Uwakala wa Umma

Uwakala wa umma ni utaratibu ambapo serikali hupata bidhaa na huduma. Utaratibu mbaya wa uwakala unaweza kusababisha bidhaa na huduma zisizo bora na matumizi mabaya ya fedha za umma. Hili huwafanya maskini kuingia kwenye hatari zaidi. Tafiti nyingi zimeonyesha kuwa kuna rushwa kubwa sana kwenye uwakala wa umma. Sheria ya Uwakala wa mwaka 2000 inajaribu kuishughulikia rushwa kwenye uwakala wa umma kwa kuweka taratibu za uwazi na utendaji.

HAKI KAZI PHDR SW 9/6/05 9:22 AM Page 38

Ukadiriaji na Ukusanyaji Kodi

Kodi ya mapato haijaongezeka kwa sababu ya msamaha wa kodi kwa mfadhili anayegharimia uingizaji na kuwepo kwa vichocheo vingi vya kodi kwa vitegauchumi vipya. Wakati huohuo, ukusanyaji wa kodi ya mapato umepanda kwa sababu ya Lipa Kadiri Unavyoingiza (PAYE) kwa waajiriwa. Rushwa pia ni tatizo. Kodi nyingi za vijijini ni mizigo mizito kwa maskini. Serikali imejaribu kupunguza mzigo huu kwa kurahisisha mfumo wa kodi na kuondoa kodi zisizo za lazima katika maeneo ya vijijini, hata hivyo hili bado halijatekelezwa kikamilifu. Serikali pia imeondoa kodi ya maendeleo mwaka 2003 na baadhi ya halmashauri za vijiji sasa zina mifumo yao ya kodi ya kuwasaidia maskini. Jitihada zaidi lazima zifanywe kuongeza misingi ya kodi kwa namna ya usawa.

Kodi ni 12% tu ya sehemu ya Pato la Taifa (GDP).

Usimamizi wa Rasilimali

Tanzania imefikia maendeleo makubwa katika uchumi wa jumla na marekebisho ya sekta za umma, ikiwa ni pamoja na ubinafsishaji wa viwanda vya umma. Hata hivyo, Watanzania wengi bado wanaishi katika hali ya umaskini ingawa uchumi umeboreshwa. Wakati watu wanaonekana kuzikubali sera za ubinafsishaji, lakini hawakubali ubinafsishaji wa maliasili, elimu na afya. Pia, kuna masuala makubwa ya uwazi katika ubinafsishaji wa viwanda vya umma.

Uwajibikaji na Uadilifu Katika Ofisi za Umma

Marekebisho mbalimbali yamefanywa kuongeza uwazi, uwajibikaji na uadilifu katika huduma za umma (angalia kisanduku). Hata hivyo, jitihada za kuendeleza uwajibikaji na uadilifu hutegemea wananchi kwa kiasi kikubwa hali ya kusimamia utendaji na kulalamika, ambayo kwa sasa ni ndogo. Kumekuwa na majaribio machache ya kuuelimisha umma juu ya sheria na kanuni zilizopo zinazotawala tabia za maofisa wa umma.

Marekebiso yanajumuisha:

- Marekebisho ya Utumishi wa Umma (1990s)
- Programu ya Marekebisho ya Utumishi wa Umma
- Maadili ya Utumishi wa Umma (1999)
- Programu ya Maboresho ya Serikali za Mitaa (LGRP)

Rushwa na Upunguzaji wa Umaskini

Serikali imefanya jitihada za kupambana na rushwa (angalia kisanduku). Nyingi ya jitihada hizi ni mpya hivyo itachukua muda kuona matokeo. Katika kiwango cha vijijini, rushwa bado imeenea sana. Kulingana na Taarifa ya Hali ya Rushwa Tanzania, rushwa imekithiri katika huduma za afya, ikifuatiwa na jeshi la polisi, leseni za biashara, mahakama, mamlaka za kodi, elimu na huduma za umma. Umma haushirikishwi kwenye mapambano dhidi ya rushwa. Unahitaji kuelezwa juu ya jitihada za kuzuia rushwa ili uchukue hatua.

Jitihada za kuzuia Rushwa:

- Uanzishaji wa Taasisi ya Kuzuia Rushwa (TAKURU)
- Wizara zimeunda mipango ya kupambana na rushwa
- Mamlaka za wilaya zimeandaa semina za kuzuia rushwa
- Vyombo vya habari vinazungumzia Mkakati wa Kuzuia Rushwa

2. Utekelezaji wa Sheria na Utawala wa Sheria

Uhusiano mkubwa kati ya utawala na upunguzaji umaskini ni kuwa na mfumo wa sheria ambao unawasaidia watu maskini kupata haki. Hata hivyo, kuna masuala yanayohitaji kubadilishwa ili watu maskini waweze kupata haki zao. Masuala haya ni pamoja na mahakama huru, kutokuwepo kwa

rushwa, msaada wa kisheria kwa maskini na kuwepo kwa mahakama. Sehemu ya chini inaonyesha vikwazo ambavyo huzuia utawala wa sheria na kuathiri maskini.

Mahakama na Utawala wa Sheria

Mahakama nchini Tanzania ziko huru, lakini kuna vitendo vingi vya rushwa, na hali hii ni mbaya zaidi kwenye mahakama za chini. Makarani wa mahakama na mahakimu wanashiriki kwenye vitendo vya rushwa. Watu huamini kuwa hawawezi kupata hukumu ya haki bila ya kutoa rushwa. Mazingira mabaya ya kazini ya watendaji wa mahakamani na rasilimali zisizotosha zinachangia rushwa na utendaji mbovu.

Tatizo jingine ni upataji wa haki. Upataji huu unahusu muda unaotumika kuendesha kesi (angalia kisanduku). Pia, watu hutumia muda mrefu na rasilimali nyingi kuwarubuni polisi, waendesha mashitaka, makarani wa mahakama na mahakimu kuwasaidia ndugu zao.

Kesi za mahakama nchini Tanzania kwa kawaida huchukua muda mrefu - jijini Dar es Salaam wastani ni muda wa miaka 3.

Watu maskini ambao hawawezi kuweka uwakili wanahitaji msaada wa huduma ya kisheria. Hata hivyo, msaada wa kisheria nchini Tanzania ni mdogo, si madhubuti na hautoshi. Kwa hakika ni wale tu wenye mashitaka yanayohusu makosa makubwa ndio wanaoweza kupata msaada wa kisheria.

Matatizo haya huathiri utawala wa sheria na kukwamisha upunguzaji wa umaskini. Utendaji wa kazi usio bora na rushwa mahakamani huongeza gharama, ambayo daima huwaangukia maskini. Programu ya Urekebishaji wa Sekta ya Sheria (LSRP) ya mwaka 1999 na mpango wake wa utekelezaji vilianzishwa kushughulikia tatizo hili. Sekta hii inakusudia kuanzisha utaratibu wa sheria ambapo hukumu kwa wakati itatolewa kwa wote, lakini itachukua muda kuona kama ina mchango wowote.

Polisi na Utawala wa Sheria

Jeshi la Polisi ni moja ya taasisi zenye rushwa zaidi (angalia kisanduku). Pia maofisa wa polisi hawatoshi. Wananchi hawana imani na polisi kwa sababu ya huduma mbovu. Wakati huohuo, watu wanaona kuwa uhalifu ni tatizo kubwa. Serikali imefanya jitihada ya kujenga vituo vidogo vya polisi katika maeneo mbalimbali. Hata hivyo, vituo hivi ni vya matukio ya dharura tu na vingi viko mijini, hivyo watu wa vijijini wanafaidika kidogo au kutofaidika navyo kabisa.

Sababu zinazosababisha rushwa kwa polisi:

- Maslahi duni
- Hali na mazingira mabaya ya kazi
- Mishahara midogo
- Watu kutoelewa haki zao

Asasi Nyingine za Utekelezaji wa Sheria

Wananchi katika jamii za vijijini wameunda vikundi vyao vya ulinzi kujilinda wenyewe. Tatizo ni kuwa vikundi hivi huchukua sheria mikononi mwao, na wakati mwingine hukataa kuwapeleka wahalifu polisi na mahakamani. Pia, wakati mwingine hushambulia na kukiuka haki za binadamu kwa kofia ya ulinzi wa jamii.

3. Kuelekea katika Demokrasia na Ushiriki

Demokrasia na ushiriki ni muhimu katika utekelezaji wa Mkakati wa kwanza wa Kupunguza Umaskini. Sehemu hii inaangalia kama maendeleo ya kuelekea demokrasia na ushiriki yameboresha hali za maskini. Programu ya Maboresho ya Serikali za Mitaa (LGRP), jumuiya ya kiraia, na vyombo vya habari zinapitiwa kwa kuhusishwa na jitihada za upunguzaji wa umaskini.

Mafanikio ya Programu ya Maboresho ya Serikali za Mitaaa (LGRP):

- Mabadiliko katika sheria na taratibu zinazoathiri uongozi wa mikoani na vijijini
- Uanzishaji wa kamati za mitaa katika halmashauri za miji zilizo karibu na watu
- Utekelezaji wa maadili wa wafanyakazi na madiwani
- Programu za elimu za kukuza uelewa wa umma kuhusu marekebisho zilitolewa

Masuala ya Utawala katika Mageuzi ya Serikali za Mitaa

Lengo la msingi la mageuzi katika serikali za mitaa ni kuanzisha utaratibu wa utawala bora wenye misingi ya uwajibikaji, taratibu za kidemokasia, na ushiriki wa umma. Programu ya Maboresho ya Serikali za Mitaa imekuwa na mafanikio kadhaa (angalia kisanduku), lakini utekelezaji umekuwa wa taratibu na haujafikia kiwango cha kata na vijiji. Halmashauri za vijiji na umma hazishirikishwi vya kutosha, na mamlaka za vijiji zina uwezo mdogo. Serikali kuu bado ina udhibiti mkubwa dhidi ya mamlaka za vijiji. Mamlaka za vijiji zinahitaji kuwa na uhuru zaidi wa kukusanya mapato na kuyatumia kulingana na vipaumbele vyao.

Jumuiya ya Kiraia

Jumuiya ya kiraia imekua sana katika muongo uliopita, jambo ambalo ni muhimu kwa demokrasia. Jumuiya ya kiraia inasaidia kuathiri sera na kufanya uhamasishaji kwa niaba ya maskini (angalia kisanduku). Hata hivyo, vyama vya kiraia viko mijini, na kuna uhusiano mdogo kati ya vyama vya kiraia na maskini walio wengi. Jumuiya ya kiraia inahitaji kuhamisha uangalizi wake kwenye ngazi za chini ili kuwa na utendaji ulio bora.

Mifano ya ushiriki wa jumuiya ya kiraia katika mchakato wa sera ya kupunguza umaskini:

- Uanzishaji wa Baraza la Sera la Asasi Zisizo za Serikali (NGO Policy Forum)
- Ushiriki wa jumuiya za wananchi katika Mapitio ya Matumizi ya Umma na Vikundi Tendaji vya Mkakati wa kwanza wa Kupunguza Umaskini

Vyombo vya Habari

Kazi muhimu za vyombo vya habari:

- Kusaidia kutekeleza uwazi na uwajibikaji
- Kusaidia kulinda dhidi ya matendo yasiyo ya haki za binadamu
- Kufanya kazi kama chombo cha kuzuia rushwa

Vyombo vya habari nchini Tanzania vimeongezeka na kupanua shughuli zake tangu katikati ya miaka ya 1990. Kama ilivyo kwa jumuiya ya kiraia, vyombo vya habari vina jukumu muhimu la kufanya katika kuimarisha demokrasia na ushirikishwaji (angalia kisanduku). Hata hivyo, vyombo vya habari vinakosa uzoefu kwa sababu kwa miaka mingi taaluma ya habari haikuendelezwa nchini. Hivyo, ubora wa vyombo vya habari vya leo ni mbovu na taaluma ya habari inakosa ujuzi wa kufanya uchunguzi wa kina. Pia, vyombo vya habari haviko huru, kwa vile vinadhibitiwa na matajiri na wenye nguvu za kisiasa na biashara. Hali hii inavizuia vyombo vya habari kuchangia kwa kina demokrasia na hivyo kwenye upunguzaji wa umaskini.



Kilimo

Sekta ya kilimo ina umuhimu mkubwa kuendeleza ukuaji wa uchumi na kupunguza umaskini nchini Tanzania. Sehemu hii inaangalia mambo ya msingi yafuatayo katika kilimo:

1. Athari za marekebisho
2. Huduma za kilimo
3. Kodi ya kilimo

HAKI KAZI PHDR SW 9/6/05 9:22 AM Page 42

1. Athari za Marekebisho

Mazao ya Chakula

Kama matokeo ya soko huria, biashara ya mazao ya chakula imeongezeka haraka. Biashara ya mazao ya chakula kwa sasa imevamiwa na vyombo binafsi, isipokuwa Hifadhi ya Nafaka ya Kimkakati (Strategic Grain Reserve). Soko hutegemea bei. Hata hivyo, wakulima bado wana wakati mgumu kuwafikia wanunuzi wa mazao wanayozalisha. Kutokana na uhaba wa masoko, wakulima wanaendelea kuuza kwa bei ya chini kwa sababu hawana usafiri wa kuchukua mazao yao nje ya vijiji na hivyo huwategemea wafanyabiashara wachache wanaofika vijijini.

Marekebisho katika Sekta ya Kilimo (tangu mwanzoni mwa miaka ya 1990):

- Soko huria la mazao ya kilimo
- Kuondoa udhibiti wa serikali
- Serikali kujitoa katika uzalishaji
- Uhuru wa sekta binafsi
- Ugawanyaji wa huduma hadi serikali za mitaa

Mazao Yanayosafirishwa Nje

Wajibu wa ushirika umeanguka vibaya. Usambazaji wa pembejeo umechukuliwa na sekta binafsi, ingawa baadhi ya vyama vya ushirika vinaendelea kufanya kazi. Katika zao la korosho, biashara huria imesababisha shughuli kubwa ya sekta binafsi na ufunguaji wa viwanda vya korosho. Hata hivyo, sehemu ya sekta iliyobinafsishwa bado ina udhaifu unaoathiri uzalishaji na masoko. Wafanyabiashara wadogo wanaozalisha mazao yanayosafirishwa nje wana uwezo wa kupata faida kubwa. Hata hivyo, wakulima wengi hawajapata faida kamili, kwa sababu ya uzalishaji usio makini na mfumo mbovu wa soko. Hili huongeza gharama, hupunguza mapato, na kuzuia upataji wa fedha za nje kwa wauzaji wa mazao ya nje.

Biashara ya Mipakani

Sera za serikali zinabainisha kuwa biashara ya mipakani itaruhusiwa, kuwezeshwa na kuhimizwa. Hata hivyo, bado kuna vikwazo vingi, hivyo wakulima hawawezi kupata bei nzuri inayotolewa kwa wakati wa uzalishaji mdogo kusaidia bei ndogo inayotolewa wakati wa vipindi vya uzalishaji mkubwa. Biashara isiyo na kibali ya mipakani nchini Tanzania inahusisha ubadilishanaji wa kiasi kikubwa cha mazao (angalia kisanduku). Mapato katika biashara hii pia yanajumuisha mchango wake katika usalama wa chakula kwa kuongeza usambazaji kwa uingizaji ndani. Hata hivyo, kodi kubwa, taratibu zinazochanganya, viwango vikubwa vya ubadilishaji wa fedha, na usumbufu wa polisi kwa wafanyabiashara ni sababu zinazokwamisha biashara ya mipakani.

Kulingana na Wizara ya Kilimo, zaidi ya tani 18,000 za mahindi zenye thamani ya dola milioni 3 husafirishwa bila kibali kila mwaka kwenye nchi jirani na Tanzania.

Upataji na Uwezo wa Kupata Pembejeo

Baada ya marekebisho, sekta binafsi sasa ina wajibu wa kusambaza pembejeo na matumizi yake nchini Tanzania yameshuka. Inaonekana kuwa wakulima hawawezi kununua pembejeo, kwani vyama vya ushirika havisambazi tena pembejeo kwa mkopo na hakuna huduma mbadala ya mikopo. Upatikanaji wa pembejeo pia husababisha vikwazo katika maeneo fulani.

Pembejeo muhimu za kilimo kwa ajili ya uzalishaji wa mazao:

- Mbolea za kikemikali
- Dawa za kuua wadudu
- Mbegu bora

Marekebisho ya soko pia yamechangia kupungua kwa upatikanaji wa pembejeo na kushuka kwa bei ya mazao katika maeneo ya vijijini. Hii ni kwa sababu ya ushiriki mdogo wa sekta binafsi katika usambazaji wa pembejeo za kilimo na ununuzi wa mazao kutoka vijijini. Licha ya kuwa ubinafsishaji ulitegemewa kuboresha usambazaji wa pembejeo vijijini, hili halikutokea. Ubinafsishaji wa soko la pembejeo umekuwa katika kiwango cha jumla katika maeneo ya mijini.

Upataji wa Mikopo

Huduma za kifedha, hasa mikopo kwa pembejeo, zimekufa kwenye maeneo ya vijijini. Benki nyingi mpya binafsi hazijarudisha vyama vya ushirika na hazizihudumii jamii za vijijini. Mipango ya mikopo midogo haijafanikiwa kwa sababu ya matatizo ya utendaji, miundo mbinu, n.k. Wakulima na wazalishaji wengi wadogo hawawezi kumudu gharama za uzalishaji na shughuli za masoko kwa kutumia pesa taslimu, hasa kwa sababu pembejeo ni ghali sana. Hawawezi kupata mikopo ya benki. Mara nyingi, wanategemea mikopo kutoka kwa vyanzo visivyo rasmi. Kwa wakati huu hakuna mikakati iliyo wazi ya serikali kwa kutoa huduma za kifedha vijijini. Mikakati mipya inahitajika kutoa huduma zinazojenga kwenye mifumo isiyo rasmi kwenye jamii za vijijini.

HAKI KAZI PHDR SW 9/6/05 9:22 AM Page 44

2. Huduma za Kilimo

Malengo ya Huduma za Kilimo:

- Kuboresha uzalishaji wa kilimo
- Kuinua pato la kilimo
- Kuboresha hali ya maisha ya wakazi wa vijijini

Usambazaji wa Huduma za Kilimo

Serikali imesambaza huduma za kilimo kwenye mamlaka za mitaa. Muundo wa maofisa wasambazaji wa mikoa na wa wilaya hawapo tena. Wakulima huwaendea washauri wa kilimo na mifugo wanapokuwa na matatizo. Chini ya utaratibu wa zamani, wataalam wa mikoani walitumiwa kuratibu programu za usambazaji kwa kila wilaya. Kwa sasa kila wilaya inatakiwa kutoa huduma za usambazaji kwa gharama yao, na halmashauri nyingi hazina vyombo, rasilimali, na uwezo wa kutoa huduma hizi. Hakuna tena mkakati wa kubadilishana taarifa katika ngazi za mikoa na wilaya, na sasa ni vigumu kupata ushirikiano mzuri kutoka vijijini.

Upataji wa Huduma za Kilimo

Kulingana na utafiti, kutembelewa na maofisa wasambazaji wa huduma za kilimo kulikuwa kidogo sana kwenye maeneo mengi. Idadi kubwa ya wakulima walipokea huduma kutoka watoaji binafsi, zaidi ya serikali au asasi zisizo za kiserikali. Utafiti pia unaonyesha kuwa muundo wa usambazaji wa pembejeo unapatikana zaidi kwa wakulima matajiri. Hili linaonyesha kuwa kuna haja ya kuweka mfumo wa pembejeo utakaowawezesha wakulima kupata pembejeo zaidi. Matajiri pia wanatumia zaidi usambazaji binafsi wa huduma, ingawa 30% ya wakulima maskini walisema wametumia usambazaji binafsi.

3. Kodi ya Kilimo

Kodi na Ada Maalum za Kilimo

Kodi kwenye mazao yanayosafirishwa nje	Kulikuwa na aina mbalimbali za kodi na ada kwa mazao yote yaliyosafirishwa nje. Mzigo wa kodi kwa wakulima ulikuwa mkubwa, kulingana na aina ya zao.
Kodi kwenye mazao ya chakula	Kodi ya uzalishaji ya wilaya ilikuwa ni kodi pekee iliyokuwepo kwa mazao ya chakula. Mazao ya chakula hayakutozwa kodi sana, ingawa kwa baadhi ya mazao kodi hizi zilikuwa za juu kwa wakulima wadogo.
Kodi kwenye mifugo	Kulikuwa na kodi, ushuru na ada nyingi kwenye mifugo: • Kodi ya mifugo na mchango wa elimu kwa kila ng'ombe anayeuzwa wilayani • Ada za soko, uhamiaji, ufugaji, safari za akiba, na ardhi iliyoshikiliwa • Ada za machinjio, ukaguzi wa nyama, na ada ya ngozi Mzigo wa kodi ulikuwa wa juu zaidi (47%) ambao ulikwamisha ukuaji wa biashara ya mifugo.
Leseni za Biashara	• Wafanyabiashara na wamiliki katika sekta ya mazao ya kusafirishwa nje wanatakiwa kulipia ada kwa leseni kadhaa.

Athari za Kodi

- **Kodi ya Serikali Kuu** ina athari ndogo kwa wakulima wengi wadogo kwani hawana kipato kikubwa kiasi cha kutakiwa kulipa kodi. Hata hivyo, huwa wanalipa kodi wanaponunua bidhaa za kibiashara au zile zinazoagizwa nje. Mashamba makubwa hulipa kodi kubwa kwa serikali kuu.

- **Kodi ya Serikali za Mitaa.** Kuna kodi mbalimbali za serikali za mitaa kwa aina zote za uzalishaji katika kilimo. Wakulima wadogo wanaozalisha mazao ya chakula yanayouzwa kwa njia zisizokuwa rasmi walilipa kodi ya maendeleo tu. Wakulima walipouza mazao ya chakula kwa njia rasmi walilazimika kulipa kodi ya wilaya, elimu na serikali za mitaa. Malipo haya yanaweza kuwa zaidi ya asilimia 10 ya thamani ya jumla ya mazao yanayouzwa, ambao ni mzigo mkubwa kwa wakulima wadogo. Wakulima wakubwa pia walilipa kodi, ingawa kodi yao ilikuwa kubwa zaidi. Wazalishaji wa mifugo pia walikuwa na mzigo mkubwa wa kodi za ndani.

- **Kodi ya Wakala wa Serikali**. Wakulima na wazalishaji wa mifugo wanaouza bidhaa zao kwa njia rasmi hulipa kodi kwa wakala wa serikali. Mzigo mkubwa wa kodi huangukia wazalishaji wa "mazao ya asili yanayosafirishwa nje." Mara nyingi mzigo wa kodi ulikuwa unatosha kuwakatisha tamaa wakulima kuzalisha aina fulani ya zao kwa sababu ya kuogopa gharama ya ziada.

Usawa wa Kodi ya Kilimo

Mzigo mkubwa zaidi wa kodi uliwaangukia wakulima waliozalisha kwa ajili ya soko bila kujali kiwango chao cha mapato au uwezo wa kulipa.

Athari za jumla za kodi ni kwamba:	**Athari zaidi ni pamoja na:**
• Zilipunguza uwezekano wa kupata masoko • Zilipunguza kilimo cha kibiashara katika ngazi zote • Zilipunguza ukuaji wa mapato na uzalishaji	• Kupunguza uhakika (utoshelevu) wa chakula • Kusababisha na kuendeleza umaskini • Kuongeza uwezekano wa kuathirika zaidi na umaskini kwa watu wa vijijini

Hitimisho

Kwa ujumla, mabadiliko yalifungua masoko kwa pembejeo pamoja na mazao. Hata hivyo, uendeshaji ndani ya soko huria haujawa na ufanisi. Mifumo ya uzalishaji na masoko bado ni dhaifu mno. Wakulima wengi bado hawajanufaika kikamilifu kutokana na uzalishaji.

Katika bajeti 2003/04, Serikali ilipendekeza kwamba kodi kwenye mazao ya kilimo isiwe zaidi ya asilimia 5 kwa mazao yaliyo shambani na bidhaa za mazao hayo zisitozwe kodi zaidi ya mara moja.

Huduma za kifedha zilizopo zinashindwa kutimiza mahitaji ya jamii za vijijini, kwa sababu zinalenga zaidi katika maeneo ya mijini. Ni mipango michache tu inayofadhiliwa na wahisani inayotoa mikopo vijijini. Mageuzi katika masoko yamehusishwa na kupungua kwa uwezo wa pembejeo na kuanguka kwa bei ya mazao. Kiwango cha ushiriki wa sekta binafsi katika kusambaza pembejeo katika maeneo haya bado ni kidogo.

Kwa ujumla, sera zilizopo husisitiza maendeleo ya kilimo na kupunguza umaskini. Hata hivyo, kumekuwa hakuna mipango ya mikakati ya kutekeleza sera hizo kwa vitendo. Hii ni muhimu katika kuleta faida/manufaa ya sera na mikakati kwa wakulima wadogo. Serikali tayari imeandaa Mkakati wa Maendeleo ya Sekta ya Kilimo (ASDS) ili kujenga mazingira ya kuboresha manufaa katika sekta na kuboresha vipato na kupunguza umaskini vijijini. Shughuli pamoja na ratiba ya utekelezaji wake vipo katika Mpango wa Maendeleo ya Sekta ya Kilimo (ASDP). Kinachosubiriwa ni kuona ni jinsi gani mpango huu utahakikisha kwamba wakulima wanapata manufaa kamili ya uzalishaji chini ya soko huria.

HAKI KAZI PHDR SW 9/6/05 9:22 AM Page 46

Changamoto, Hitimisho na Mapendekezo

MASOMO NA CHANGAMOTO

Tofauti za Umaskini

Umaskini umeenea kote Tanzania na huathiri wananchi wengi. Hata hivyo ni muhimu kutambua kwamba umaskini unatofautiana sana kiviwango. Hii ina maana kwamba umaskini unajionyesha tofauti tofauti kulingana na vigezo mbalimbali. Kwa mfano kuna tofauti za umaskini kati ya:

- Maeneo ya mijini na vijijini
- Mikoa mbalimbali ya nchi
- Wanaume na wanawake
- Kaya zenye viwango tofauti vya mapato

Kwa sababu ya tofauti hizi, ni hatari kuangalia viwango vya wastani vya nchi katika kupima upunguaji wa umaskini. Ni muhimu kuangalia tofauti hizi kwa ukaribu zaidi na kuwa na taarifa zilizopo ambazo hutuonyesha ni kwa jinsi gani upunguzaji wa umaskini huathiri makundi mbalimbali. Hii itasaidia kuona kama upunguzaji wa umaskini ni sawa kwa makundi yote. Somo lingine ni kwamba kuna njia nyingi za kufikia malengo ya upunguzaji wa umaskini, na baadhi ya njia hizi zinafaa zaidi kuliko nyingine. Lengo la kitaifa linaweza kufikiwa kwa uboreshaji kwa watu wote au kwa uboreshaji mkubwa zaidi kwa sehemu au baadhi ya wananchi. Usawa utaongezeka au kupungua kutegemeana na mkakati uliotumiwa.



Mambo haya hufanya tujiulize kama njia ya "kiwango kimoja hufaa kwa wote" ni sahihi kwa Mkakati wa Kupunguza Umaskini, ambao hutumika kwa nchi nzima na makundi yote ya jamii. Kwa vile umaskini unatofautiana, mikakati ya kupunguza umaskini inabidi itofautiane zaidi. Hili linaweza kufanyika kwa njia mbili:-

1. Watunga sera wangelenga katika makundi maalum na/au mikoa wanapokuwa wanarekebisha mikakati ya upunguzaji wa umaskini. Hii ingesaidia katika mgawanyo wa rasilimali.
2. Mikakati ya kupunguza umaskini inahitaji kutafsiriwa kwa vitendo katika ngazi ya mamlaka za mitaa. Hii ingesaidia kulenga katika mahitaji maalum ya jamii.

Mwisho, utaratibu wa ufuatiliaji wa umaskini uboreshwe ili uweze kupata taarifa za makundi maalum na wanaonufaika zaidi na mikakati ya kupunguza umaskini. Hii inahitaji uimarishaji wa ukusanyaji taarifa na uchambuzi makini zaidi wa taarifa zilizopo.

Kufanya Ukuaji wa Uchumi Uwajali Maskini

Kuna mikakati mikuu miwili katika kufanya ukuaji wa uchumi uwajali zaidi maskini:
1. Hakikisha kwamba sekta zinazokuwa kwa kasi zinatoa manufaa makubwa zaidi kwa maskini
2. Sisitiza ukuaji zaidi katika sekta hizo ambazo zina athari zaidi kwa watu maskini

Katika Tanzania sekta za madini na utalii zimekua haraka sana katika miaka ya karibuni. Hata hivyo, sekta hizo hazijasaidia vya kutosha katika kupunguza umaskini. Kwa mfano sekta ya utalii ilitoa ajira kwa asilimia 1 tu, ingawa ilichangia asilimia 14 katika Pato la Taifa mwaka 2000. Uhusiano wake na sekta nyingine ni finyu, hivyo jamii za wenyeji hunufaika kidogo mno na kuongezeka kwa uwekezaji katika utalii. Hali hii ni sawa na sekta ya madini, ambapo wawekezaji toka nje hunufaika kutokana na misamaha ya kodi. Sekta ya madini hunufaisha uchumi katika ngazi ya juu mno. Hata hivyo, katika ngazi ya jamii, manufaa hutokana tu na misaada ya hisani inayotolewa na makampuni ya uchimbaji madini katika maeneo yanayozunguka migodi hiyo. Uchimbaji mdogomdogo una manufaa zaidi hasa katika kutoa ajira. Hata hivyo, ni ajira ya hatari, isiyo na usalama na isiyotambulika kisera. Sera zinahitaji kuhusisha sekta za madini na utalii na sekta nyingine ili ziweze kutoa ajira zaidi na kutoa manufaa ya moja kwa moja kwa jamii za asili.

Mwisho, ni muhimu kuhakikisha kwamba sekta ambazo hutoa ajira kwa watu wengi walio maskini kama vile kilimo zinakua kwa kasi zaidi. Kilimo ni muhimu katika kupunguza umaskini. Mkakati wa Maendeleo ya Sekta ya Kilimo (ASDS) na Mkakati wa Maendeleo Vijijini (RDS) inalenga katika kuboresha kilimo na kupunguza umaskini katika maeneo ya vijijini. Hata hivyo, ni mapema mno kuweza kujua kama mikakati hii itaongeza ukuaji wa kilimo na kunufaisha maskini.

HITIMISHO

Ukuaji wa uchumi wa jumla haujaweza bado kuboresha ustawi wa maskini. Kwa hiyo, sera lazima zihakikishe kuwa faida ya ukuaji wa kiuchumi yafike kwa watu maskini.

Umaskini wa Kipato

Yafuatayo ni mambo makuu yanayojitokeza katika suala la umaskini wa kipato:

- *Ukuaji wa uchumi wa jumla haujaweza bado kuboresha ustawi wa maskini.* Sera lazima zilenge katika kupunguza umaskini vijijini na kuunganisha na kuimarisha uchumi wa jumla na uchumi katika ngazi ya jamii.

HAKI KAZI PHDR SW 9/6/05 9:22 AM Page 48

- *Kilimo kinazidi kudidimizwa na pembejeo na matatizo ya kimfumo.* Kutegemea kilimo cha mvua ni tatizo kubwa. Matatizo ya usafirishaji huathiri ugawaji wa chakula kutoka maeneo yenye ziada kwenda katika maeneo yenye upungufu. Usafirishwaji wa mazao nje haukuwa mzuri katika miaka ya karibuni. Mapato yameshuka kwa sababu ya kuanguka kwa uzalishaji na bei za mazao. Kuna madai kwamba ubora wa mazao hayo pia umeshuka.

- *Miundo mbinu dhaifu na barabara.* Matengenezo ya barabara za vijijini hayaridhishi. Kulenga katika matengenezo ya mara kwa mara badala ya kuboresha barabara kumechangia kuwa kikwazo kikubwa kwa watu maskini vijijini kufikia masoko na kupata pembejeo wanazomudu kununua.



Umaskini Usio wa Kipato

Elimu

Mambo muhimu yanayojitokeza ni kama ifuatayo:

- Kulikuwa na maendeleo mengi sana katika elimu ya msingi, hasa katika uandikishwaji wa watoto kwa sababu ya Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Msingi (MMEM).
- Mikakati ya kupunguza umaskini inaweza ikawa imelenga zaidi katika uandikishwaji badala ya kuboresha elimu. Idadi ya wanaoacha shule ni kubwa, kiwango cha kufaulu kinabakia kuwa cha chini hasa kwa wasichana na kiwango cha wasichana kujiunga na elimu ya juu kinabaki kuwa chini.

Maeneo muhimu katika elimu:

- Ubora
- Wanafunzi kuendelea na shule hadi kumaliza
- Usawa wa kijinsia
- Kiwango cha kufaulu
- Kiwango cha uandikishwaji katika ngazi za sekondari na vyuo

Kuishi, Lishe na Afya

Mambo muhimu yanayojitokeza katika kuishi, lishe na afya yanaonyesha mchanganyiko. Mipango ya chanjo ya watoto na tiba ya kifua kikuu ilionyesha mafanikio, lakini kulikuwa na mabadiliko kidogo katika maeneo mengine ya afya katika miaka ya 1990. Mambo mengine muhimu ni kama ifuatavyo:

Kuna tofauti kubwa kati ya hali ya afya ya matajiri sana (20%) na maskini sana (20%) na kati ya maeneo ya mijini na vijijini.

- Viwango vya vifo vya watoto wadogo na wachanga havijashuka tangu miaka ya 1980.
- Uthibitisho Unganifu wa Magonjwa ya Kitoto (IMCI) umefanikiwa katika kuboresha uwezekano wa watoto kuishi. Kwa hiyo, watoto wachanga na wale walio chini ya umri wa miaka 5 wana viwango vya vifo vinavyoendana na malengo ya Mkakati wa kwanza wa Kupunguza Umaskini yaliyoainishwa mwaka 2003.
- Maambukizo ya VVU/UKIMWI yanaendelea kuongezeka. Hii itaendelea kuathiri ustawi wa jamii na ukuaji wa uchumi.
- Lazima kukata mwenendo wa miaka ya 1990 ili kufika malengo ya lishe kwa watoto ya Mkakati wa kwanza wa Kupunguza Umaskini. Lishe kwa wanawake wajawazito, unyonyeshaji na ulishaji uliopo sasa kwa watoto wadogo lazima vizingatiwe na kuboreshwa.

Maji na Usafi

- Ingawa kumekuwepo na ongezeko katika matumizi ya maji ya bomba katika maeneo ya vijijini, matokeo yanaonyesha kwamba kaya za watu maskini zinaweza kutumia maji yasiyo salama kuliko kaya za watu wasio maskini.

Utawala

Mambo muhimu katika utawala ni:

- Hapajakuwa na ongezeko la kawaida katika asilimia ya wilaya zenye taarifa safi za ukaguzi wa fedha/hesabu.
- Ushughulikiaji wa kesi za rushwa unafanyika polepole mno kiasi cha kuwafanya watu wakate tamaa kutoa taarifa hizo.
- Uwajibikaji wa serikali katika ngazi za chini kuanzia juu ni dhaifu.
- Vyama vya kiraia vimeongezeka katika miaka ya 1990, kitu ambacho kinaweza kuchangia katika utawala bora, uwajibikaji, uwazi na utawala wa sheria.

Mageuzi ya serikali za mitaa hayajafikia jamii na kata ambapo ndipo wananchi wengi huishi. Hii inakwamisha ushiriki wa pamoja.

MAPENDEKEZO

Udhaifu wa Taarifa

Kutokuwepo kwa taarifa za kitaifa za hivi karibuni ni moja kati ya vikwazo katika kuchambua umaskini kikamilifu kwa sasa.

- Vingi kati ya viashirio vya kudhibiti umaskini haviwezi kuonyesha mabadiliko ndani ya miaka 3 na lazima vipimwe kwa muda mrefu zaidi.
- Uchunguzi wa VVU/UKIMWI na Uchunguzi wa Kilimo (2003) zitaonyesha taarifa/takwimu zaidi na kuwezesha uchambuzi mzuri zaidi wa viashirio hivi.
- Uchunguzi wa kuonyesha kwenye sehemu gani umaskini uko nchini Tanzania (Poverty Mapping Study) utotoa taarifa nzuri katika tofauti za kijiografia katika umaskini wa kipato.
- Mifumo ya taarifa za mara kwa mara inahitaji kuboreshwa ili kutathmini mabadiliko katika upunguzaji wa umaskini kwa mwaka.
- Mfumo wa Usimamiaji wa Taarifa za Afya na taarifa za maji na usafi zingeweza kuboreshwa kwa kuongeza ubora wa taarifa.
- Ufuatiliaji lazima utumie vyanzo vingine vya taarifa/takwimu vilivyo nje ya mifumo ya uchunguzi ya kitaifa, ikiwa ni pamoja na Mapitio ya Matumizi ya Umma (PER) na kutoka katika mifumo ya udhibiti ya sekta husika.

Maeneo yasiyo na taarifa:

- Kilimo
- Afya
- Umaskini uliokithiri
- Utawala
- Uhusishaji wa umaskini na mazingira

HAKI KAZI PHDR SW 9/6/05 9:22 AM Page 50

Usawa

Masuala yanayohusiana na ukuaji na upunguzaji wa umaskini na kuongezeka kwa pengo la usawa kati ya makundi mbalimbali yanahitaji kushughulikiwa kwa upya na kuzingatiwa.

- Tathmini ya Mkakati wa kwanza wa Kupunguza Umaskini inahitaji kuangalia ugawaji wa manufaa kutokana na ukuaji, kwa vile kuna ongezeko la pengo kati ya maskini na wasio maskini.
- Kutenga rasilimali zaidi kwa ajili ya kilimo ni njia moja ya kufanya ukuaji unaowajali maskini ambayo pia ingeongeza rasilimali kwa barabara mbovu vijijini.

Kuna ongezeko la pengo kati ya maskini na wasio maskini katika Tanzania.

Mambo Yahusuyo Ubora wa Elimu ya Msingi

Jitihada zaidi zinatakiwa kuboresha ubora, kiwango cha kufaulu na usawa wa kijinsia.

- Washiriki katika Wiki ya Sera ya Umaskini walishauri kamati za shule zifuatilie viwango vya ukatishaji masomo.
- Jitihada za kuwashirikisha wale wenye umri mkubwa lazima zifanyike kwa kuimarisha Mpango wa Elimu ya Msingi kwa Waliokosa (MEMKWA).
- Kufanya vibaya kwenye masomo kwa wasichana kunahitaji kushughulikiwa haraka na pia mabadiliko katika mazingira ya shule na fikra za watu.

Wajumbe katika Wiki ya Sera ya Umaskini walishauri kwamba bajeti itolewe kwa usawa ili kuhakikisha kunakuwa na *wingi na ubora katika elimu* (mfano **wingi** ni kama kuongeza madarasa n.k. na **ubora** ni kama mtaala mzuri/bora na kuboresha walimu.

Huduma za Afya ya Msingi

- Kuongezeka kwa gharama za afya kumewatenga maskini.
- Sera ya msamaha wa ada za huduma hizo iliyopo haifanyi kazi kabisa.
- Suala hili lazima kuangaliwa kwa makini na kufanyiwa kazi haraka.

Gharama za huduma za afya zimewafanya maskini kushindwa kupata huduma hizo.

Maambukizi ya VVU/UKIMWI

- Kupunguza maambukizi kutoka kwa mama kwenda kwa mtoto lazima kupewa kipaumbele.
- Vituo vingi vya huduma za afya havina madawa ya kutosha kwa ajili ya wagonjwa wa VVU na UKIMWI kwa hiyo badala yake watu watumie huduma za majumbani.
- Lazima kuwepo na mfumo wa kuwasaidia wale walioko katika hatari zaidi kupitia mipango ya kinga ya jamii kwa sababu ya madhara ya VVU/UKIMWI.
- Mipango ya kifedha inayowezekana kwa ajili ya mipango ya kinga ya jamii inahitajika kuangaliwa.

Utawala

- Utawala haujashirikishwa vya kutosha kwenye Mkakati wa kwanza wa Kupunguza Umaskini kwa sababu ya upatikanaji dhaifu wa takwimu au taarifa na viashirio sahihi ili udhibiti mwendelezo wake.
- Kuna haja ya kuainisha mambo ya kiutawala yanayoathiri watu maskini na ambayo huzuia uwezo wao katika kupata huduma za msingi (mf. rushwa).
- Kuna haja ya kuwa na mfumo fanisi wa kudhibiti na kuimarisha ukusanyaji wa takwimu au taarifa kuhusu viashirio vya utawala.

HAKI KAZI PHDR SW 9/6/05 9:22 AM Page 51

Maana ya Baadhi ya Maneno Magumu

Athari za umaskini — Huu ni msamiati unaotumika kuelezea mtu, kaya au jamii wanapokuwa katika uwezekano wa kuathirika zaidi na umaskini kuliko walivyo sasa.

Faida inayotarajiwa — Huu ni msamiati unaotumika tunapoangalia madhara mbalimbali ya matumizi ya umma kwa kaya zenye viwango tofauti vya kiuchumi. Kwa maana nyingine hii inamaanisha nani anafaidika kutokana na matumizi ya umma.

Gharama za Ulaji (CPI) — CPI inapima mabadiliko katika gharama za kuishi mwaka hadi mwaka kwa kuzingatia vitu kama gharama ya chakula, makazi na usafiri.

Idadi ya uzazi — Wastani wa watoto ambao mwanamke huzaa katika maisha yake.

Idadi ya vifo — Idadi ya watu wanaokufa ikilinganishwa na jumla ya watu waliopo. Hii inaelezwa kwa idadi ya vifo kwa kila watu elfu moja.

Mapitio ya Matumizi ya Umma (PER) — Hii ni mfumo ambao hujumuisha maofisa wa serikali, wawakilishi wa biashara, mashirika ya kijamii na washirika wa kimaendeleo kwa lengo la kuangalia jinsi serikali inavyokusanya na kutumia fedha zilizopitishwa kwenye bajeti. Mapitio ya mara kwa mara hufanyika ili kuhakikisha kwamba fedha zinatumika vizuri katika maeneo yaliyopewa kipaumbele.

Mfumuko wa bei — Ni kipimo cha kiwango cha ongezeko la bei mwaka hadi mwaka.

Mstari wa umaskini wa chakula — Huu unatafsiriwa kulingana na kiwango cha chini cha kipato kinachohitajika kukidhi mahitaji ya lishe ya mtu. Hiki ni kiwango cha chini zaidi cha umaskini kuliko kile cha umaskini wa mahitaji ya msingi.

Mstari wa umaskini wa mahitaji ya msingi — Hiki ni kiwango cha chini kinavyotafsiriwa kulingana na kiwango cha chini kinachohitajika ili kukidhi mahitaji ya msingi ya mtu.

Nguvu za umaskini — Mishtuko na mashinikizo zinazowaingiza watu, kaya au jamii katika umaskini.

Pato la Taifa (GDP) — Ni kipimo cha jumla ya mali zilizozalishwa katika nchi, yaani jumla ya thamani ya bidhaa na huduma zote zilizozalishwa na kubadilishwa kwa fedha.

Sekta binafsi — Hii hujumuisha mashirika yote yasiyo ya kiserikali, k.m. biashara.

Sekta za umma — Mashirika yote ya kiserikali.

HAKI KAZI PHDR SW 9/6/05 9:22 AM Page 52

Soko huria

Hii ina maana kwamba serikali imeondoa vizuizi katika uchumi ili uchumi uwe huru. Kwa maneno mengine ina maana kwamba uchumi utategemea na mwenendo wa soko na kwamba sekta binafsi ndio inayoongoza ukuaji wa uchumi.

Taarifa

Kuna aina mbili za taarifa kwenye ripoti hii. Moja ni taarifa zinazotokana na hoja na idadi (yaani takwimu) na zinazoeleza *nini* kinatokea kwenye hali maalum. Aina ya pili ni taarifa zinazotokana na uzoefu, mitazamo, na maoni ya watu. Taarifa hizi zinatusaidia kueleza *kwanini* mambo yanatokea kwenye hali maalum.

Uangalizi wa jamii

Hii ina maana ya kuwalinda maskini na wale walio katika hatari ya kuathirika zaidi, kwa kuwasaidia katika kukidhi mahitaji yao ya lazima pale wanaposhindwa kujimudu.

Uchumi wa jumla

Inaangalia uchumi mzima wa nchi yaani jinsi ambavyo mali inazalishwa na kugawanywa. Inaangalia thamani ya uzalishaji, ukosefu wa ajira, ongezeko la bei na mzunguko wa biashara. Pia huangalia uhusiano kati ya sekta mbalimbali za uchumi. Malengo makuu ni ajira kamili, kuimarika na ukuaji wa uchumi.

Ukuaji wa uchumi wa jumla

Hii inaamanisha kusimamia uchumi ili kuepuka mabadiliko makubwa katika uzalishaji, ajira na hasa bei. Ni matokeo ya kuwa na sera bora zinazoweka na kutekeleza malengo yaliyo na manufaa kwa nchi katika kipindi maalum. Sera hizi hubuniwa ili kuwezesha ukuaji wa uchumi.

Umri wa kuishi

Wastani wa miaka watu wanayotarajia kuishi.

Usambazaji wa madaraka

Kutoa mamlaka na uwajibikaji toka serikali kuu kwenda ngazi za chini za utawala. Watu wengi zaidi wanaposhirikishwa katika maamuzi, usimamizi na utoaji wa huduma katika ngazi zote, kuna nafasi kubwa ya kuwa na maendeleo thabiti, endelevu na ya usawa.

Ustawi

Hii ni ile hali nzuri ya mtu inayotokana na kutoathirika na hali zote zinazosababisha umaskini. Hujumuisha ubora wa hali zote ikiwemo mali, afya na jamii. Na pia usalama na uhuru wa kufanya maamuzi na vitendo vinavyofaa.

Utawala

Ni jinsi ambavyo madaraka yanatumiwa na serikali katika kusimamia rasilimali za kijamii na kiuchumi za nchi. Utawala bora ni matumizi ya madaraka kwa uadilifu, usawa, uwazi na uwajibikaji. Utawala bora unamaanisha kwamba hakuna rushwa na serikali inaheshimu sheria na haki za watu.

HAKI KAZI PHDR SW 9/6/05 9:22 AM Page 53

SHUKRANI

Kitabu hiki ni mwongozo ulioandikwa kwa lugha rahisi wa Taarifa za Umaskini na Maendeleo ya Watu (PHDR) mwaka 2002 na 2003 na unaonyesha nia ya serikali katika kuhamasisha ushiriki mpana zaidi katika kupanga, kutekeleza na kutathmini sera na mikakati ya kupunguza umaskini.

Kitabu hiki ni matokeo ya kazi za watu na mashirika mbalimbali. Shukrani hizi zinatambua na kutilia maanani kazi za watu hao na mashirika hayo hususani wale waliohusika moja kwa moja katika kutoa mwongozo huu.

Shukrani maalum ziwaendee wanachama wa Kundi la Utafiti na Uchambuzi (R&AWG) ambao walitoa maoni ya manufaa juu ya kazi za awali ya kitabu hiki ili kuhakikisha kwamba zilikuwa sahihi na timilifu.

Mwisho, shukrani za kipekee ziende kwa Hakikazi Catalyst ambao walijishughulisha kikamilifu katika kutoa toleo hili. Shukrani nyingine ni kwa Nathan Mpangala kwa katuni zake zinazosisimua.

Design and Printing:
Colour Print (T) Ltd.

Taarifa ya Umaskini na Maendeleo ya Watu ni moja ya matokeo muhimu ya Utaratibu wa Ufuatiliaji wa Umaskini. Hii ni nyenzo inayotumiwa na serikali kutafiti kama Mkakati wa kwanza wa Kupunguza Umaskini una athari zozote katika kupunguza umaskini. Upimaji wa kupunguza umaskini unajumuisha utumiaji wa viashirio ambavyo vimeonyeshwa kwenye Mkakati wa kwanza wa Kupunguza Umaskini. Mkakati huu unaelezea maeneo ya vipaumbele katika kupunguza umaskini na kupanga malengo, shughuli na viashirio vya kupunguza umaskini. Taarifa ya Umaskini na Maendeleo ya Watu inachambua kiwango cha umaskini katika sekta za kipaumbele kwa kutumia viashirio hivi. Ufuatiliaji wa maendeleo ya upunguzaji wa umaskini ni sehemu muhimu ya utekelezaji wa Mkakati wa kwanza wa Kupunguza Umaskini na Taarifa ya Umaskini na Maendeleo ya Watu ni sehemu ya utaratibu huu.

Kwa maelezo zaidi wasiliana na:

Kitengo cha Kuondoa Umaskini
Ofisi ya Makamu wa Rais
Mtaa wa Mkwepu
S.L.P. 5380
Dar es Salaam
Simu: 022-2113857
Tovuti: www.povertymonitoring.go.tz

Research on Poverty Alleviation (REPOA)
Mtaa wa Mgombani 157
Regent Estate
S.L.P. 33223
Dar es Salaam
Simu: 022-2700083 / 2772556
Baruapepe: repoa@repoa.or.tz
Tovuti: www.repoa.or.tz